SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

UKURASA 2



## Magereza watoa ufafanuzi mfungwa, mahabusu kupigwa risasi Mtwara


MAISHA
FEBRUARI 13, 2022
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili
Ukurasa 14
Katlesi ya nyama kiburudisho tosha
MAISHA NI NYUMBA
Namna ya kupamba chumba siku ya Valentine
Ukurasa 15
KATUNIKA
Ukurasa 16
VALENTINE DAY
Mavazi yanayoonyesha mapenzi mazito
Ukurasa 13

UKURASA 9

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumapili Februari 13, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0580855
www.ippmedia.com
JUMAPILI
www...com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango

# 'Vigogo' kitanzini uharibifu mazingira

**Wamo** mawaziri, wawekezaji wakubwa. Dk. Mpango asema 'msinitafute ubaya'... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Mkurugenzi wa Kituo cha Kuwezesha Wajasiriamali cha F Start Up, Roxanne Varza, na Meneja Mawasiliano wa Kituo hicho, Grégoire Martinez, kuhusu kazi mbalimbali zinazofanywa kituoni hapo, zikiwamo kutoa fursa kwa wajasiriamali wadogo kupata elimu ya ubunifu wa kibiashara, fursa za mitaji yenye masharti rafiki pamoja na masoko, alipokitembelea jijini Paris, Ufaransa jana. **PICHA: IKULU**

## Wafukua kaburi baada ya kubaini wamezika maiti ya asiyehusika

UKURASA 3

# Waziri ataka majina polisi wasio waadilifu

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA YATAMBA ASEC HAWAPONI UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Magereza wafafanua mfungwa, mahabusu kupigwa risasi

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Magereza limetoa ufafanuzi kuhusu mfungwa na mahabusu kupigwa risasi mkoani Mtwara.

Kwenye toleo la Nipashe jana, katika ukurasa huu, kulikuwa na habari yenye kichwa cha habari 'Mfungwa, mahabusu wauawa kwa kupigwa risasi wakijaribu kutoroka', ikibainisha kuwa mfungwa aliyekuwa akitumikia kifungo cha miaka 30 gerezani na mahabusu aliyekuwa na tuhuma za mauaji, walifariki dunia kwa kupigwa risasi na askari wa Jeshi la Magereza wakati wakijaribu kutoroka kwenye Gereza Kuu la Lilungu mkoani Mtwara.

Tukio hilo linadaiwa kutokea Desemba 17 mwaka jana majira ya saa sita mchana likimhusisha mfungwa mwenye namba 321/2021 Juma Mohamed Mwanya na mahabusu Dionis Robat mwenye namba za mahabusu 469/2020, aliyekuwa ameshtakiwa kwa kosa la mauaji katika Mahakama ya Wilaya ya Lindi.

Hata hivyo, Mkuu wa Jeshi la Magereza Mkoa wa Mtwara, Kamishna Msaidizi Raymond Mwampashe, aliiambia Nipashe jana kuwa kilichotokea si mauaji, bali wawili hao walifariki dunia wakati wakipelekwa hospitalini baada ya kupigwa risasi walipokaidi kutii amri ya askari wa jeshi hilo.

Alifafanua kuwa askari walilazimika kuwadhibiti kwa kutumia silaha wawili hao baada ya kuwa wamekaidi amri iliyotolewa ikiambatana na kufyatua risasi angani baada ya kumshambulia kwa kitu kizito usoni askari Bamila Maneno.

Katika ufafanuzi wake kwa Nipashe juzi kuhusiana na tukio hilo, Mwampashe alisema: "Kwa taarifa nilizoletewa, walifanikiwa kuruka ukuta wa ngome ya magereza muda huo wa mchana na askari wetu waliposhtuka wakapiga filimbi kwa ajili ya kuwazingira lakini walishatoka nje ya gereza na kukimbilia kwenye mashamba ya korosho, hivyo jitihada za kuwatafuta zilianza mara moja kwa askari kuzunguka kila eneo huku wawili wakienda na pikipiki kuzuia barabara kuu," alidai.

Aliongeza kuwa wakati msako ukiendelea askari magereza waliokuwa na pikipiki walikutana na askari wa usalama barabarani na walipowauliza kama wamewaona wafungwa wakipita katika eneo hilo, wakawaambia wameona watu wawili wamepita wakiwa wanakimbia baada ya kuvuka barabara ya kuelekea Newala.

Alidai kuwa baada ya taarifa hiyo, askari walizunguka msitu uliokuwa karibu na eneo waliloelekezwa na wakati msako ukiendelea mwenzao mmoja alipigwa na kitu kizito na mmoja wa waliotoroka huku wakimfuata askari mwenye silaha ili kumpokonya.

Mwampashe aliongeza kuwa hata walipoambiwa wajisalimishe walikataa na wakawa wanazidi kuwakabili askari ndipo walipigwa risasi kisha wakachukuliwa kwa ajili ya kuwahishwa Hospitali ya Ligula baada ya taratibu za kipolisi katika eneo hilo kukamilika, lakini walifariki dunia kutokana na kuvuja damu nyingi.

Kwa mujibu Mwampashe, mahabusu alikuwa na kesi ya tuhuma za mauaji katika Wilaya ya Lindi na alihamishiwa Gereza Kuu la Lilungu Oktoba 9 mwaka jana akiwa anatumikia kifungo cha miaka miwili baada ya kujaribu kutoroka wakati akisubiri kesi yake ya mauaji iendelee huko Lindi.

Alisema mfungwa Mwanya aliyejaribu kutoroka alikuwa kwenye kifungo cha miaka 30 gerezani baada ya kuhukumiwa na Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Ruangwa Julai 26 mwaka jana kutumikia adhabu hiyo alipokutwa na hatia ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

"Huyu Mfungwa mwili wake tuliwakabidhi ndugu zake lakini mahabusu alizikwa na manispaa baada ya jitihada za kutafuta ndugu zake huko mikoa ya kanda ya ziwa kushindikana," alidai.

*Jeshi la Magereza limetoa ufafanuzi kuhusu tukio hilo kutokana na mkanganyiko wa baadhi ya mambo yaliyokuwamo katika habari ya jana... **Mhariri**



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (katikati), akizindua Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021, jijini Dodoma jana. Kushoto ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Suleiman Jafo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji, Viwanda, Biashara na Mazingira, David Kihanzile. **PICHA: OMR**

# Vigogo kitanzini uharibifu wa mazingira

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameagiza mawaziri watano kwenda kufanya tathmini ya uharibifu wa mazingira katika vyanzo vya Mto Rufiji hususani Bonde la Ihefu ambako amebaini kuna viongozi na wawekezaji wakubwa wanachangia uharibifu huo.

Mawaziri hao ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro.

Dk. Mpango alitoa agizo hilo jana alipozindua Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 jijini hapa.

Aliagiza mawaziri hao waende kwenye maeneo hayo baada ya mkutano wa Bunge unaoendelea kwa sasa na wawasilishe taarifa ya tathmini hiyo kwake pamoja na hatua walizochukua.

"Niwaombe sana kamati yetu ya Bunge mlisimamie, hili ni jambo muhimu sana lenye maslahi mapana kwa taifa letu, mimi sipo tayari kama Makamu wa Rais kuona tunakamilisha ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere halafu baadaye maji hayapatikani kutokana na uharibifu unaofanyika katika vyanzo vyote vya Mto Rufiji," alisema.

Makamu wa Rais alisema shughuli za kilimo na mifugo ni muhimu katika ukuaji wa uchumi lakini ni lazima zifanywe bila kuvunja sheria za uhifadhi wa mazingira.

"Kwa mfano kwenye chanzo cha Mto Ruaha katika Bonde la Ihefu kule Mbeya, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa kamwambie jirani yako na wewe mwenyewe hakikisheni kuna matumizi endelevu ya mto huo na mingine.

"Nina fahamu hata baadhi ya viongozi wanahusika, hawa ni viongozi wenye mfano mbaya, wana makundi makubwa ya mifugo ndani ya Bonde la Ihefu, wengine ni wawekezaji wakubwa, wana mashamba makubwa ya mpunga na wanaelekeza maji kwenye mashamba yao kiholela bila utaratibu wa kuyarudisha mtoni," alisema.

**ONYO LA DODOMA**

"Dodoma kumekuwa na ukataji wa miti holela kwa ajili ya mkaa, kwenye eneo la chanzo cha maji Mzakwe... sasa hapa natoa onyo serikali haitaendelea kulifumbia macho suala hili, maana inashangaza pale Zamahelo kuna kizuizi cha kukagua mazao ya misitu lakini kila jioni kuna misafara ya pikipiki isiyoisha inaleta magunia jijini Dodoma na askari wapo wanaangalia tu, na wengine wanakusanya mapato mifukoni mwao.

"Hili pia nimeliona katika maeneo ya Mkoa wa Pwani kuanzia Mlandizi hadi Kibaha kuelekea jijini Dar es Salaam, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na TFS (Wakala wa Huduma za Misitu) mkomeshe na mhakikishe mnakomesha uharibifu wa mapori tengefu nchini kote," aliagiza.

Pia alimwagiza Waziri wa Ofisi yake, Dk. Selemani Jafo kusimamia uundaji wa timu itakayokuwa chini ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma itayarishe mpango mkakati wa 'kukijanisha' na kusafisha Mji wa Dodoma na apate mpango huo ndani ya siku 30 kwa kuwa anataka Dodoma iwe kama Singapore na taarifa ya utekelezaji iwasilishwe kwake kila baada ya miezi mitatu. "Utekelezaji utakapokuwa unalegalega, wahusika wawajibike wenyewe kabla sijaingilia kati, natumaini wamenisikia, Waziri wa TAMISEMI anagusa kila mkoa, hakikisheni hili linafanyika na kuanzia sasa katika ziara zangu ajenda yangu ya kwanza itakuwa ni kufanya mkoa au wilaya kuwa ya kijani na safi nikikuta pachafu mtakuwa mnanitafuta ubaya,"alisema.

**DAR KINARA USAFI**

Alipongeza Jiji la Dar es Salaam kwa kuwa jiji la sita kwa usafi katika majiji ya Afrika kwa mujibu wa jarida la 'Tour Africa' huku akitaja Manispaa za Moshi na Iringa kuongoza kwa usafi nchini.

Pamoja na hayo, alisema suala la uhifadhi wa mazingira ikiwamo upandaji miti ni ajenda ya kudumu kwa taasisi za serikali na zisizo za serikali na kwamba hicho ni kipimo kwa kila kiongozi.

"Taarifa ya hali ya mazingira nchini 2019 ilionyesha kuna upungufu mwingi kuhusu namna tunavyotekeleza sera na sheria zinazohusu hifadhi na usimamizi wa mazingira. Kwenye taarifa ile inasema kumekuwa na ongezeko la uharibifu wa ardhi ambao unahusiana na shughuli za ufugaji, kilimo na ukataji wa miti ovyo.

"Kiwango cha uharibifu wa ardhi kimeongezeka kutoka asilimia 42 mwaka 1980 hadi asilimia 50 mwaka 2012 na kufikia asilimia 63 mwaka 2018, hii maana yake kama taifa hatuna budi kuimarisha mipango mikakati ya utekelezaji,"alisema.

Aliagiza kusimamiwa upandaji miti kwa kila kaya na maeneo yote ya taasisi za serikali na zisizo za serikali huku akiagiza Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) na Wakala wa Barabara (TANROADS) kusimamia makandarasi kupanda miti kwenye kila barabara inayojengwa.

Awali Dk. Jafo alisema sera iliyozinduliwa itaongeza fursa katika urejeshaji wa takangumu kwa matumizi mbalimbali na imezingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji, Viwanda, Biashara na Mazingira, David Kihenzile, alisema kuna uhitaji wa upandaji wa miti trilioni 1.7 Tanzania na kamati itahakikisha inalipa kipaumbele suala hilo na kuwa mabalozi kwa wananchi.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alisema watahakikisha barabara zote za mitaa 222 zinatambulishwa kwa kupandwa miti pamoja na kuondoa miti isiyofaa eneo la Nyerere Square na kupanda miti inayoendana na hadhi ya eneo hilo.

Alisema wananchi wa mkoa huo wanatakiwa kupanda miti mitano kila kaya ikiwamo miwili ya matunda na kuahidi kusimamia utekelezaji wake.

## Wafukua kaburi baada ya kuzika maiti isiyohusika

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

KATIKA hali isiyo ya kawaida, ndugu wamelazimika kufukua kaburi katika kata ya Kilakala, Manispaa ya Morogoro baada ya kubaini familia ilichukua mwili wa mtu mwingine katika chumba cha kuhifadhi maiti cha Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro na kwenda kuizika.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Bigwa Sokoni, kata ya Kilakala, Jastine Mkoba, akisimulia mkasa huo jana, alisema mwili huo ulizikwa Februari 10 mwaka huu lakini siku iliyofuata familia nyingine iliibuka na kuudai mwili uliozikwa ni wa ndugu yao.

Alisema aliyefariki dunia katika mtaa wake ni Gervas Chondoma lakini mwili ambao waliuzika ni wa mtu mwingine.

Alisema Chondoma alifariki dunia Februari 9 mwaka huu na siku iliyofuata walimzika lakini siku mbili baada ya maziko, yaani Februari 11, watu wanne walimfuata wakidai mwili uliozikwa katika mtaa huo ni wa ndugu yao.

"Nilikataa kwa sababu nami ni sehemu ya familia ya marehemu (Chondoma), niliwaambia twende wote chumba cha kuhifadhi maiti, tulipita msibani nikamchukua kijana wa marehemu, tulipoonyeshwa mwili mtoto wa marehemu alimtambua kuwa ni baba yake," alisema.

Alisema baada ya kuutambua mwili huo, ndipo walipopewa maelekezo ya kuirudisha hospitalini huko maiti iliyokuwa imeshazikwa.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa kutokana na hali hiyo, kama kiongozi aliamua kwenda polisi kuomba mwongozo wa namna ya kufanya, nako alitakiwa arudi hospitalini ili kupata kibali cha kufukua kaburi.

"Nilikwenda chumba cha kuhifadhi maiti na kuwaeleza wahudumu wake, akaniambia halina shida kwa sababu bahati nzuri wenyewe (ndugu wa marehemu hao) majina yamefanana na ni ukoo mmoja kwa hiyo wamezikana ndugu kwa ndugu. Kwa hiyo (ndugu) walikaa wakakubaliana wabadilishe miili," alisema.

Mkazi wa Bigwa Sokoni, kata ya Kilakala, Khamis Ibrahim, alisema wakati wa kwenda kuchukua mwili wa Chondoma, alikuwa miongoni mwa watu waliokwenda. "Kabla ya kuzika asubuhi nilishiriki kwenda kuchukua mwili hospitalini, tulipofika chumba cha kuhifadhi maiti tuliona mwili ni wa mzee, nilikwenda na suti, wahudumu wakamvika na tukamweka kwenye jeneza tukiwa na mtoto wa marehemu pamoja na mdogo wa marehemu," alisema.

Khamis alisema baada ya kuzika Februari 10, mwaka huu siku iliyofuata wakati akielekea kwenye shughuli zake alikutana na Mwenyekiti wa Mtaa na kumweleza kuwa mzee aliyezikwa siyo.

Mdogo wa marehemu, Mohamed Mkwama alisema kilichotokea ni makosa madogo ya waliokwenda hospitalini kuchukua maiti.

Jana alipotafutwa na Nipashe Jumapili kuzungumzia tukio hilo, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Dk. Daniel Nkungu, alisema: "Hospitali haijapokea malalamiko yoyote kutoka kwa ndugu wa marehemu kuhusu suala hili. Busara ni kuongea na ndugu wa marehemu pande zote."



Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Masauni akikagua gwaride la wahitimu wa mafunzo ya wakaguzi wasaidizi wa Polisi, katika kambi ya Kilelepori, Wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro jana, ambapo askari 1,955 wamehitimu mafunzo hayo. **PICHA: WMNN**

# Waziri ataka majina polisi wasio waadilifu

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, amemwagiza Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Simon Sirro, kumpatia majina ya askari polisi wanaojihusisha na matukio yasiyo ya maadili ili awashughulikie.

Amesema lengo la kuwashughulikia askari hao wasio waadilifu, ni kusaidia kuwa na jeshi imara, safi na linaloaminika kwa jamii.

Akizungumza wakati akifunga mafunzo ya wakaguzi wasaidizi wa polisi katika Kambi ya Polisi ya Kilelepori wilayani Hai mkoani Kilimanjaro jana, Masauni alisema yeye ni Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi ambayo inashughulikia nidhamu ya askari, hivyo atawashughulikia skari hao ambao hawana nidhamu.

"Katika kipindi hiki mimi ni Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi, kama kuna askari ambaye atakuwa anafanya vitu vya ovyo, IGP mlete tu tumalizane naye, hatuwezi kucheka na vitu ambavyo havina maslahi na tija katika nchi hii, tutaendelea kusimamia kweli kweli nidhamu, ni kwa dhamira njema kwa wengi ninyi mlio safi," alisema.

Masauni aliongeza kuwa nidhamu ya askari ni muhimu katika Jeshi la Polisi kwa kuwa wanategemewa katika jamii na pia wananchi wana imani kubwa na askari, hivyo inasikitisha kuona askari anaenda kuua raia au askari anatoa siri, akisisitiza jambo hilo halikubaliki ndani ya jeshi hilo.

"Inasikitisha leo kunakuwa na askari anaenda kuua raia, hata kama ni mmoja, inasikitisha kuna askari leo anapora, askari anabambikia kesi mtu, aibu na dhambi kubwa, askari anatoa siri kwa wahalifu, lazima tufuate maadili, hili halikubaliki na tutawashughulikia wanaofanya matukio hayo, lazima tusimamie nidhamu ya jeshi," alionya.

Masauni pia alizungumzia matukio ya dawa za kulevya na udhalilishaji hasa upande wa Zanzibar, akiwataka askari waliohitimu mafunzo hayo watakaopangwa katika kata mbalimbali nchini, kwa watakaopangwa Zanzibar wahakikishe wanapambana na matukio hayo.

Waziri huyo pia alisema matukio ya mauaji yanayoendelea nchini pamoja na baadhi ya polisi wanaojihusisha na matukio ya uhalifu yanamfanya akose usingizi, hivyo akawataka askari kuwa waadilifu.

Aliongeza kuwa tangu ateuliwe kuiongoza wizara hiyo takriban mwezi mmoja sasa, matukio ya mauaji pamoja na baadhi ya askari polisi kushiriki katika masuala ya uhalifu, yanamkosesha usingizi na hata Rais Samia Suluhu Hassan naye anakosa usingizi kutokana na matukio hayo.

"Mimi tangu nimeingia ndani ya wizara hii kwa kipindi hiki cha muda mfupi kama mwezi mmoja hivi, kuna vitu wiwili vikubwa vinanikosesha sana usingizi, na si mimi tu nina uhakika Amiri Jeshi Mkuu Rais Samia Suluhu Hassan, naye anakosa usingizi.

"Na pia na Watanzania wote walio wema, wazalendo, wanaoipenda nchi yao, watakuwa wanakosa usingizi. Matukio hayo la kwanza ni mauaji, mara utasikia kachinjwa mtu, ukiuliza sababu unaambiwa sababu ya mapenzi, mara kaenda kwa mganga kadhulumiwa, pamoja na sababu nyingi tu," alisema Masauni.

IGP Sirro alisema zipo changamoto kama uhalifu unaovuka mipaka, ugaidi na makosa ya dawa za kulevya ambazo kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama vitendo hivyo vimeendelea kudhibitiwa.

Alikiri kwamba zipo dosari nyingine ikiwamo mmomonyoko wa maadili kwenye jamii.

"Mheshimiwa waziri, tunaendelea kupambana na uhalifu unaovuka mipaka, ugaidi na makosa ya dawa za kulevya kwa kushirikiana na vyombo vingine ya ulinzi na usalama, pia bado zipo changamoto nyingine ikiwamo mmomonyoko wa maadili kwenye jamii," alisema IGP Sirro.

Mkuu wa Shule ya Polisi Moshi mkoani Kilimanjaro, Ramadhani Mungi, alisema jumla ya wanafunzi 1,955 wamehitimu mafunzo ya Mkaguzi Msaidizi wa Polisi na wahitimu hao wamejifunza mbinu mbalimbali za kukabiliana na makosa ya uhalifu na wahalifu.

# Mchuchuma, General Tyre zazua jambo bungeni

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

BUNGE limeitaka serikali kutoa msukumo kwenye miradi ya kimkakati ya Liganga na Mchuchuma, huku likionyesha kutoridhishwa na uamuzi wa kubadili matumizi ya eneo la kiwanda cha matairi cha General Tyre. Hayo yalisemwa juzi bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, David Kihenzile, wakati akiwasilisha taarifa ya kamati hiyo.

"Bunge linaazimia kwamba, kwa miradi yote ya kimkakati inayotekelezwa na Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC), ipewe msukumo katika utekelezaji wake. Mfano mradi wa Liganga na Mchuchuma majadiliano yanayoendelea baina ya serikali na mbia kampuni ya Sichuan Ltd.

"Yamechukua muda mrefu kumalizika na serikali inapaswa kumaliza majadiliano hayo, ili mradi sasa uanze kutekelezwa na wananchi waweze kunufaika na uwapo wa rasilimali hizi katika maeneo yao," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema serikali inapaswa kulipa fidia wananchi ambao ardhi yao ilitwaliwa kupisha utekelezaji wa miradi bila kusubiri miradi husika kuanza.

"Mkwamo huo katika utekelezaji wa miradi unaleta hasara kwa serikali na kuchelewesha maendeleo ya nchi katika ukusanyaji kodi, ajira na uchagizaji wa uchumi wa jamii zinazozunguka miradi hiyo," alisema.

Aliongeza kuwa kamati imeona serikali inahitaji kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi inayosimamiwa na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

Mwenyekiti huyo alisema miradi ya kimkakati ya Liganga na Mchuchuma, Mradi wa Magadi Soda ya Engaruka na Mradi wa Kiwanda cha Matairi cha Arusha bado hakuna jambo lililokamilika.

"Kamati haijawahi kuridhishwa na mwenendo wa suala la mradi wa Liganga na Mchuchuma ambao haujaanza hadi muda huu ambao taarifa hii inaandaliwa. Mara kwa mara Wizara imekuwa ikija na habari mbalimbali juu ya mradi huu.

"Mara nyingi ni taarifa za kujirudiarudia ambazo kamati haioni mwendelezo wake na kutoona umakini au nia ya dhati ya serikali katika kufanya mradi huu uanze au kuachana na mwekezaji wa kampuni ya Sichuan Ltd.

"Katika mkutano wa mwisho wa mwezi Februari mwaka huu baina ya kamati na wizara, wizara imeahidi jambo hili linakwenda kuisha muda si mrefu kwa mwekezaji kuanza kazi au kuvunja mkataba naye.

"Kamati inaishauri serikali kuweka nguvu na jitihada kumaliza majadiliano haya ambayo yamechukua muda mrefu kumalizika.

"Jambo ambalo linachelewesha taifa letu kupata mapato ya kodi, ajira kwa vijana na ahueni kwa wananchi wa Wilaya ya Ludewa ambao wanahitaji kufidiwa kutokana na maeneo yao kuchukuliwa na mradi huu," alisisitiza.


## KUPOTEA KWA CHETI



116703602

**NIKO ANYIGULILE MWAKALINGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato che nne chenye index namba **S.3466-0435** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia WAILES SEKONDARI mwaka 2011. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CHA/RB/61750/2022.**

# Watetezi wa haki washtuka lugha mgogoro Ngorongoro

**Na Beatrice Shayo**

WATETEZI wa haki za binadamu nchini wameliomba Bunge kusimamia mijadala ya wabunge kuhusiana na mgogoro wa Ngorongoro kwa usawa na kukemea lugha zisizo na utu kwa wananchi waliojitoa sadaka kwa miaka mingi kulinda rasilimali katika eneo hilo.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam kwa niaba yao na Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THDRC), Onesmo Ole Ngurumwa, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusiana na mgogoro wa ardhi Wilaya ya Ngorongoro.

Alisema ni muhimu jambo hilo likatazamwa kwa upana katika pande zote kwa kuheshimu haki za wananchi hao kwa kuwa kuna upotoshaji unaoendelea kwa vyombo mbalimbali vya habari wakiwamo wabunge na watu wenye mamlaka.

Ole Ngurumwa alisema wananchi hao wanatakiwa kulipwa fidia kubwa kwa kuwa wameshiriki kwa miaka mingi kulinda hifadhi hiyo na kuzuiwa kufanya shughuli zote za kiuchumi. Alisema mgogoro wa ardhi katika Wilaya ya Ngorongoro ni wa muda mrefu na juhudi zilizofanyika kupata suluhu ya kudumu zikionekana kushindwa kuzaa matunda.

"Kabla ya kupata uhuru jamii za kifugaji zilipoteza ardhi yao huko Serengeti na kuhamishiwa maeneo ya Tarafa ya Ngorongoro na Loliondo na kuahidiwa hawataondolewa katika maeneo yao," alisema.

Aliongeza kuwa Wilaya ya Ngorongoro ina jumla ya kilometa za mraba zaidi ya 14,000 na zaidi ya asilimia 75 ya eneo hilo kwa sasa hutumika kwa shughuli za utalii na uhifadhi.

Ole Ngurumwa alisema matamshi yamewahukumu wananchi wanyonge bila hatia yoyote kwa kuwa hakuna kosa walilofanya hadi sasa kwa kuwa wapo kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Eneo la Ngorongoro ya mwaka 1959 katika hifadhi hiyo.

Alisema watetezi wa haki za binadamu wanamwomba Waziri Mkuu kuwapa nafasi wadau huru kama vile wananchi wa Ngorongoro, watetezi wa haki za binadamu na wadau wengine kushiriki katika kutoa elimu kwa wabunge kuhusu hali halisi ya Wilaya ya Ngorongoro.

Alisema wanaikumbusha serikali kuzingatia kuwa mwaka 1959 hifadhi ya Ngorongoro ilipoanzishwa ilikuwa na malengo makuu matatu yaani uhifadhi, kulinda maslahi ya wenyeji walioondolewa Serengeti kwa mkataba na wakoloni na utalii.

Ole Ngurumwa alisema maslahi hayo yaliingizwa katika Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro wakati wa wakoloni na yameendelea kuwapo katika sheria ya sasa ya mamlaka ya hifadhi hiyo.

Alishauri sheria inayounda mamlaka, ipitiwe upya na kuboresha usimamizi na ulinzi wa haki za wananchi na kuhakikisha hifadhi inalindwa na kuendelezwa.



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Halima Bulembo (katikati), akiijaribu moja ya pikipiki mpya zilizotolewa kwa mkopo kwa vikundi vya vijana kupitia mkopo wa asilimia 10 wa Sh. milioni 92, uliotolewa na Halmashauri ya Wilaya hiyo, kwa vikundi vya ujasiriamali 14 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, wilayani humo jana. Kulia kwake ni Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Issa Msumari, na (kushoto kwake) ni Ofisa Maendeleo ya Jamii wilaya, Vije Mfaume na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Erasto Mhina.

## Serikali yatoa milioni 870/- Pori la Pande

**Na Christina Haule**

PORI la Akiba Pande lililoko chini ya Mamlaka ya Usimamizi Wanyamapori Tanzania (TAWA), limepokea Sh. milioni 870 kwa mwaka wa fedha 2022/23 kutoka serikalini kwa ajili ya kuweka miundombinu ya utalii ili kuongeza watalii kwenye pori hilo.

Meneja wa pori hilo, Honest Buletta, alisema juzi ofisini kwake mkoani Dar es Salaam kuwa kwa sasa wameshaanza ujenzi wa nyumba za kulala wageni mbili, vyoo, maji, barabara ya kuzunguka mipaka ya hifadhi na eneo la 'picnic' moja, unaotarajiwa kukamilika baada ya miezi mitatu.

Alisema ukarabati huo utawasaidia katika kupunguza au kuondoa kero mbalimbali ikiwamo watalii kupata shida kwa kukosa sehemu za kupumzika hasa nyakati za mvua wakiwa hifadhini, kukosa vyoo na hivyo kulazimika kurudi maeneo ya ofisini kupata huduma zingine. Meneja huyo alisema kuwa baada ya ujenzi na ukarabati huo, watalii watakuwa wakipata huduma hizo na nyingine muhimu katika maeneo ya utalii huku ukarabati huo pia ukiongeza idadi ya watalii kutoka 100 hadi kufikia 1,000 kwa mwezi.

Aliwataka wakazi wa Jiji la Dar es Salaam kutembelea pori hilo, akitamba kuwa wakiwa ndani yake, watajiona kama hawapo kwenye mji huo kutokana na kuwa na msitu mnene uliojaa vivutio. Ofisa Uhifadhi wa Pande, Mustapher Buyagera, aliwataka wakazi wa jiji hilo la kibiashara mikoa jirani kufika kwenye pori hilo kufanya utalii wa aina mbalimbali ikiwamo kutembea kwa miguu kwa umbali wa km zaidi ya 14 na kuendesha baiskeli msituni sambamba na kujionea mimea, ndege, wanyamapori wadogo.

Buyagera alisema mbali na uboreshaji wa miundombinu hiyo, wanajiandaa kubuni aina nyingine ya utalii ikiwamo kuendesha boti bwawani, michezo ya mpira wa pete, kuendesha farasi kwa kuzunguka mipaka ya hifadhi, na kuanzisha programu ya kuchoma nyama pori. Pia alisema wana mpango wa kuweka eneo la zuio na kuweka wanyama wakubwa na wakali kwa ajili ya maonyesho kwa watalii badala ya kuwaacha hifadhini kutokana na udogo wa hifadhi hiyo iliyo katikati ya makazi ya watu.

Alisema mtalii akifika Pande, anapaswa kulipia Sh. 10,600 kama tozo kwa Mtanzania na mgeni atalipa dola za Marekani 20 na kwa watoto ni Sh. 700 na wageni ni dola 10.

Kufika Pori la Akiba Pande kutoka Kata ya Bunju mkoani Dar es Salaam hadi hifadhini ni kilometa 14.

# Waliokamata washukiwa wa mauaji watunukiwa

**Rose Jacob,** MWANZA

MAOFISA 21 wa Jeshi la Polisi mkoani Mwanza wametunukuwa vyeti na fedha taslimu kwa kufanikisha kukamatwa watu wanaodaiwa kufanya mauaji ya watu watatu wa familia moja, dereva teksi na mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT).

Mauaji hayo yalitokea hivi karibuni jijini Mwanza na jeshi la polisi lilifanya upelelezi na kuwakamata watuhumiwa.

Akizungumza wakati wa kukabidhi zawadi hizo juzi, Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Ramadhani Nganzi, alisema wamewapa tuzo hizo kutokana na namna walivyofanya kazi kwa haraka na kuwapata watuhumiwa.

Alisema kuwa mwezi uliopita watu watatu wa familia moja waliuawa katika eneo la Mecco jijini Mwanza na polisi walianza upelelezi wa haraka na kuwakamata watuhumiwa.

Aliongeza kuwa katika tukio lingine ambalo lilitokea mwezi huu, dereva teksi aliuawa wilayani Sengerema pamoja na mwanafunzi wa SAUT ambaye alipigwa na wananchi wenye hasira kwa madai kwamba alikuwa kibaka.

Aliwaomba wananchi kuliamini jeshi hilo kwa kuwa linafanya kazi nzuri kuhakikisha linatimiza majukumu yake ya kisheria ya kulinda usalama wa watu na mali zao.

Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala, ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, katika tukio hilo, alishukuru jeshi hilo kwa namna lilivyofanya kazi.

Pia aliwashukuru wananchi na wenyeviti wa serikali za mitaa kwa namna walivyoshiriki kuhakikisha watuhumiwa wanakamatwa.

Aliwaomba watu wanaotaka kwenda Mwanza kuwekeza katika biashara mbalimbali, wasisite kufanya hivyo kwa kuwa mkoa huo upo salama.

Viongozi wa Kamati ya Amani ya Mkoa wa Mwanza waliwataka polisi kwenda katika madhehebu yao kusali badala ya kufanya bila kumwomba Mungu.

Walisema Mungu ndiye anayewaongoza katika kazi zao, hivyo hawana budi kwenda kumwomba kila wanapopata nafasi.

Akizungumza katika hafla ya utoaji zawadi hizo, Sheikh wa Mkoa wa Mwanza, Hassan Kabeke, alisema suala la amani lilikuwapo tangu enzi za Mtume Mohammed na kwamba polisi wasichoke kulinda amani.

# Aomba kupatiwa mguu wa bandia

**Na Mwandishi Wetu**

MARTHA Chigogolo, mkazi wa Ndanda wilayani Masasi mkoani Mtwara, ambaye mguu wake umekatwa baada ya kuugua kisukari, anaomba msaada wa mguu wa bandia utakaomwezesha kurejea katika shughuli za kujiingizia kipato.

Akizungumza na Nipashe jana, mama huyo wa watoto wawili wanaomtegemea, alisema alikatwa mguu mwishoni mwa mwaka jana.

"Nilikatwa mguu huu mwishoni mwa mwaka jana na sasa ninatumia magongo yanayonisaidia kutembea, kabla ya kukatwa mguu, nilikuwa ninauza samaki ili kujiingizia kipato lakini kutokana na tatizo hili la mguu nimeshindwa kuendelea," alisema.

Martha alisema alikuwa akifanya biashara hiyo kwa kwenda kuchukua samaki mjini Mtwara na kwenda nao Ndanda kuwauza kwa kuwatembeza.

"Ninaomba msaada wenu ili nipate mguu ili niweze kuendelea na shughuli zangu za kila siku na kuwasomesha watoto wangu, kwa yeyote atakayeweza kunisaidia kupata mguu, namba yangu ni **0673698847**, Mungu awabariki," alisema.





Ofisa Msimamizi Mkuu wa Kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Edwin Iwato (kushoto), akitoa elimu ya taratibu za forodha zinazotumika kuwahudumia wafanyabiashara wa kati na wadogo wanaotumia Kituo cha Huduma kwa Pamoja Mpakani Sirari, wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi ya mlango kwa mlango inayoendelea mkoani Mara, jana. **PICHA: TRA**

# Waziri Aweso atishia kufumua Mfuko wa Maji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amesema hatasita kufumua Mfuko wa Maji kama hautaweka utaratibu mzuri wa kulipa fedha huku akiwaonya makandarasi watakaofanya ubabaishaji kwenye miradi ya maji nchini.

Aweso alitoa kauli hiyo juzi jijini hapa kwenye halfa ya kushuhudia utiaji saini wa mikataba 86 ya miradi ya maji chini ya Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

"Baadhi ya makandarasi wananyanyasika, upo ubabaishaji wa makusudi. Unakuta mtu amefanya kazi na anastahili alipwe haki yake, basi alipwe!

Sielewi inakuwaje mkandarasi amepata hati za malipo na huku mmeleta amelipwa, unafika mkoani anaanza kuambiwa kwamba itabidi kwanza ufanyiwe ukaguzi, ukaguzi wa nini tena? Hayo ndio magumashi ambayo yanapoteza imani,"alionya.

Alisema kuwa juzi alishtukiza kwenye mfuko wa maji na kubaini wanagawa fedha lakini hawajui kinachofanyika kwenye miradi.

"Wekeni mfumo mzuri na nitaufumua na kuweka utaratibu mzuri ili mtu akiwasilisha hati ya malipo apewe fedha aende kufanya kazi," alisema.

Waziri Aweso aliwataka makandarasi ambao wamepata hati za malipo lakini wanafanyiwa alichokiita magumashi na baadhi ya watendaji, kumtumia ujumbe ili kushughulika na wanaofanya hivyo.

Pia alitaka ushirikishwaji wa wananchi na wabunge katika kutekeleza miradi hiyo huku akiwataka mameneja wa RUWASA mikoa kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa miradi hiyo na wasipofanya hivyo wataondolewa kwenye nyadhifa hizo.

Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA, Clement Kivegalo, alisema miradi hiyo ina thamani ya takriban Sh. bilioni 309.9. Ni kati ya miradi 138 iliyotangazwa na wakala huo.

Alisema RUWASA imepanga kutekeleza miradi 1,527 na kati yake, miradi 351 ilikuwa ya utafutaji wa vyanzo vya maji na usanifu wakati miradi 1,176 ni miradi ya ujenzi wa miundombinu.

Kivegola alisema sehemu ya miradi 1,176 ni miradi ambayo imeibuka mwaka wa fedha uliopita ambayo ni 317 huku miradi mipya ikiwa ni 462 wakati miradi ya ukarabati na upanuzi ni 397.

Akifafanua hali ya utekelezaji wa miradi hiyo, alisema ipo miradi 317 iliyovuka mwaka, miradi 249 imekamilika na inatoa huduma ya maji wakati miradi 397 ya ukarabati na upanuzi ambayo inatekelezwa kwa mfumo wa 'force account' na miradi 301 imekamilika na kutoa huduma ya maji.

# Maboresho miundombinu umeme yakamilika

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Umeme (TANESCO) limewahakikishia Watanzania kupungua kwa tatizo la kukatika kwa umeme baada ya marekebisho ya miundombinu ya nishati hiyo yaliyokuwa yanafanyika kwa siku 10 kukamilika.

Februari Mosi mwaka huu shirika hilo lilitangaza mgawo wa umeme katika baadhi ya maeneo nchini ambao ulidumu hadi Februari 10.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Dar es Salaam, Msemaji wa TANESCO, Martine Mwambene, alisema marekebisho hayo yalikuwa yanafanyika Songosongo yakilenga kuongeza uwezo wa kusambaza gesi ya kutosha.

"Tuliandaa mikakati ya muda mfupi na mrefu na moja ya mikakati hii ni kuongeza uwezo wa kituo cha Kinyerezi I kutoka megawati 150 hadi 350, lakini pia ni kuamsha kituo cha ubungo namba tatu ambacho kilitarajiwa kuongeza megawati 112 ambazo mpaka sasa megawati 60 zimeshaingizwa kwenye gridi. "Katika marekebisho yaliyokuwa yanafanyika kule Songosongo kama shirika tulitumia fursa ya kurekebisha miundombinu yetu kama kubadilisha nguzo zilizochakaa kutoa za miti na kuweka za zege, kubadilisha nyaya zilizochoka, maboresho ya Transfoma na kuongeza nguvu ya uwezo wa umeme," alisema Mwambene.

Aliongeza kuwa huenda katika kipindi cha matengenezo kuna baadhi ya watu waliathirika zaidi, akidai kuwa hiyo ilitokana na sababu za kiufundi ambazo zilikuwa nje ya uwezo, huku akiwaomba radhi Watanzania kwa ujumla kwa usumbufu uliojitokeza.

"Siku hii ya leo 'jana' tumeona tuuhabarishe umma kwamba matengenezo haya yamekamilika, lakini haina maana kwamba siku ikatokea umeme ukakatika ukasema kwamba mbona ulisema mgawo umeisha, nipo hapa kufafanua kwamba matatizo ya umeme yana vyanzo mbalimbali.

"Vyanzo hivyo vinaweza vikawa ni upande wa uzalishaji au usambazaji kwahiyo mteja anategemea apate huduma ya umeme lakini unapokatika yeye hawezi kufahamu kwamba tatizo liko sehemu gani, niwahakikishie kwamba eneo ya uzalishaji liko vizuri na tuna umeme wa kutosha," alisema Mwambene.

Pia alisema kuwa nyakati zingine kunaweza kutokea hitilafu mbalimbali katika miundombinu yao na kusababisha changamoto, akitoa wito kwa wateja wao kuwa endapo wataona umeme umekatika katika eneo lao watoe taarifa kupitia namba za vituo vyao vya dharura.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Onyo la madaktari kuhusu matumizi ya P2 lizingatiwe

**ZIMEKUWAPO** taarifa kwamba kumekuwa na matumizi holela na ya kupitiliza ya vidonge vya kuzuia mimba (P2) ambayo imesababisha Chama cha Madaktari Tanzania (MAT) kutoa kauli juu ya vitendo hivyo.

Katika taarifa yake juzi, chama hicho kupitia Rais wake, Dk. Shadrack Mwaibambe, kilikemea vitendo hivyo ambavyo kwa kiasi kikubwa vinafanywa na vijana wa kike kwa lengo la kujilinda na ujauzito. Katika onyo lake, MAT ilisema vidonge hivyo vina madhara makubwa katika homoni za vijana hao kwa kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kupata matatizo ya uzazi.

MAT ilitoa onyo hilo baada ya juzi Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, kubainisha ongezeko la matumizi ya vidonge hivyo hasa kwa wasichana wenye umri unaoanzia miaka 14 hadi 24. Kutokana na taarifa hiyo, Dk. Mwaibambe aliweka bayana kwamba matumizi holela ya vidonge hivyo huchangia kuharibu mzunguko wa mwezi wa mwanamke.

Alisema matumizi ya muda mrefu ya vidonge hivyo si salama kwa watumiaji hasa wasichana wenye umri mdogo kwa kuwa inaonyesha dhahiri kwamba wanajihusisha na ngono zembe katika umri ambao wanatakiwa kujikita zaidi katika masomo. Aidha, matumizi hayo yanaonyesha kwamba wasichana hao hawachukui tahadhari dhidi ya magonjwa ya kuambukiza ikiwamo Ukimwi.

Licha ya kuonya matumizi ya vidonge hivyo, Dk. Mwaibambe pia alitoa ushauri kwa wasichana juu ya matumizi ya dawa hizo kwa kuwataka wasifanye papara kujiingiza katika masuala ya mapenzi katika umri mdogo bali wasubiri muda utakapofika.

Pamoja na hayo, MAT ilitoa angalizo kwamba kuwapo kwa watumiaji wa P2, kunabainisha kuwa wahusika wana elimu ya kujikinga na ujauzito lakini ikaenda mbali zaidi kwa kusema kuna uwezekano liko kundi lingine lisilo na elimu hiyo ambalo halitumii kinga katika ngono, hivyo linajihusisha pia na utoaji mimba.


Kama ilivyotahadharisha MAT, matumizi ya P2 yana athari kubwa kwa afya hususan mzunguko wa hedhi kwa wasichana, elimu inapaswa kutolewa ili wachukue tahadhari hasa kwa kujiepusha na vitendo vya ngono katika umri mdogo. Hii inatokana na ukweli kwamba watakapofikia umri wa kuolewa wanaweza kupata matatizo katika mzunguko wa hedhi na hata kukosa uzazi kutokana na matumizi ya vidonge hivyo.

Elimu pia inapaswa kutolewa dhidi ya matumizi ya dawa hizo kwa sababu zinaweza kusababisha matatizo makubwa ya kiafya kama vile saratani ya mlango wa kizazi na ile ya matiti ambazo ndizo zinazowapata wanawake wengi kwa sasa. Tunasema hivyo kwa sababu matumizi ya dawa bila mpango ni moja ya sababu za kuenea kwa saratani, ukiacha za ulaji na mitindo ya maisha.

Jambo lingine ambalo linapaswa kufanywa ni kwa vyombo vya dola ambavyo vimepewa dhamana ya kutekeleza sheria katika kuwadhibiti na kuwachukulia hatua wanaume wanaojihusisha na vitendo vya ngono na wasichana wenye umri wa miaka 14. Watu hao wanapaswa kuchukuliwa hatua kwa sababu ni kinyume cha sheria. Kujihusisha na vitendo hivyo na watoto wa umri huo ni ubakaji.

Ni wazi kwamba, kama alivyosema Rais wa MAT, msichana wa miaka 14 ni mtoto hata maumbile hayajakomaa na miongoni mwa watu wanaofanya ngono na watoto hao ni kama wanafanya vitendo hivyo na watoto wao wa kuwazaa. Mashirika ya kutetea haki za wanawake na watoto wachukue hatua kwa kutumia taarifa ya kamati ya bunge na angalizo la MAT.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kukwamisha miradi ni kurudisha nyuma maendeleo ya nchi yetu

Na Sabato Kasika

**SERIKALI** imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali kwa lengo la kuharakisha maendeleo ya ukuaji wa kiuchumi wa nchi ambao unatarajiwa kuipeleka katika uchumi wa kati ifikapo 2025.

Kuwapo kwa miradi ya maendeleo kuanzia vijijini, kunachangia kukuza na kutoa fursa za kiuchumi ikiwa ni pamoja na kutoa ajira, ingawa kumekuwapo na sintofahamu inayotokana na ufujaji wa fedha za miradi hiyo.

Katika ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan ya hivi karibuni mkoani Mara, alibaini kuwapo kwa ufujaji wa fedha za miradi ya maendeleo zinazotolewa na serikali na kusababisha utekelezaji wa miradi hiyo kukwama.

Uwapo wa 'madudu' hayo ni wazi kwamba mkoa hauwezi kupiga hatua kwenda mbele badala yake unabaki kama ulivyo na hali ambayo inaufanya uendelee kubaki nyuma kimaendeleo.

Nionavyo ni kwamba umefika wakati sasa wananchi kujengewa uwezo ili wawe wanafuatilia fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya maendeleo katika maeneo yao, ili wajue ni kiasi gani, kwa ajili ya miradi gani na zinatumikaje.

Hatua hiyo inawasaidia kujua utekelezaji wa miradi kama unalingana na kiasi cha fedha kilichotumika, ili kama itabainika kuwapo kwa 'madudu', basi wafikishe taarifa kwa vyombo husika ikiwamo TAKUKURU.

Mafunzo ya ufuatiliaji wa fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya maendeleo (PETS) ambayo hufanyika maeneo mbalimbali nchini, yanatosha kuwa msaada kwa wananchi kuelewa umuhimu wa ufuatiliaji wa miradi hiyo.

Ninaamini kwamba mafunzo kama hayo yanaweza kuwaamsha wananchi na kuwa makini kwa kufuatilia hatua kwa hatua miradi mbalimbali inayotekelezwa katika maeneo yao ili kuona kama inalingana na kiasi cha fedha kilichotumika.

Kupitia PETS, wananchi wanatakiwa kujua fedha za ujenzi wa majengo ya umma, barabara na miradi mingine, ni muhimu ziwe wazi, kuanzia siku ya kwanza ya kutangaza zabuni pamoja na ufunguzi wake. Wananchi wakielimishwa, na kupewa fursa ya kuchagua miradi waitakayo na kushirikishwa na pia kuwapo kwa kumbukumbu za ujenzi na matumizi katika kila eneo, hatua hiyo inaweza kusaidia kumaliza ufujaji wa fedha za umma.

Kimsingi ni kwamba, ufujaji wa fedha za umma, unakwamisha maendeleo ya wananchi na nchi kwa ujumla, hivyo ni vyema wananchi wakashiriki kikamilifu kuanzia mwanzo hadi kukamilika kwa miradi husika.

Ufujaji wa fedha za umma ulioibuliwa na Rais mkoani Mara, ni vyema ukawa fursa kwa viongozi wa mikoa mingine nchini kujifunza jambo na kuweka mikakati ya kuhakikisha hakuna senti ya umma inayoliwa.

Kama alivyoagiza Rais kuwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), isisubiri taarifa ya ukaguzi ndipo ifanye uchunguzi, ni wazi hatua hii itazuia ufujaji huo badala ya kusubiri kosa litendeke kwanza.

Ikumbukwe kwamba, karibu maeneo mengi ya nchi, mawaziri wanapokuwa katika ziara za kukagua miradi ya maendeleo, wamekuwa wakikutana na malalamiko hasa ya utekezaji wa miradi hiyo chini ya kiwango. Lakini ninaamini, wananchi wakielimishwa kupitia pets, hawatalalamika, badala yake watakuwa wanafuatilia miradi ya maendeleo katika maeneo yao kwa karibu, hali ambayo itawafanya wafujaji kuogopa.

Kwa ujumla ni kwamba, rushwa si tu adui wa haki, bali pia inachelewesha maendeleo, hivyo kila mbinu zingefanyika zikiwamo za kuelimisha wananchi kujua wajibu wao katika kusimamia miradi ya maendeleo katika maeneo yao.

Wananchi, TAKUKURU na wadau wengine wanatakiwa kushirikishwa tangu mwanzo wa mradi, kama njia mojawapo ya ufuatiliaji ili iwe rahisi kubaini kasoro kama ubora wa mradi haulingani na gharama iliyotumika.

SAFU/MAKALA

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Usiri wa nini katika wosia?



Na Pascal Mayalla

**Licha ya kutoa wosia wa kauli kwa kaka yake, siku ya siku akaita tena watoto wake wote, akaelekeza ichukuliwe kalamu na karatasi na kutoa wosia wa wazi na huku mtu akiandika kila kitu, iwapo kuna jambo litamtokea huyo kaka yake.**

KWA vile wiki iliyopita nilizungumzia shujaa mmoja mwanamke, aliyetangulia mbele ya haki, leo naomba kuzungumzia jambo moja muhimu lililojitokeza kutokana na msiba ule ambalo haliko kisheria, lakini Watanzania tukiamua kulifuata, litatusaidia sana. Ni jambo ambalo lina maslahi makubwa kwa taifa kupunguza kama si kuondoa kabisa migogoro ya mirathi. Hili ni jambo kuhusu usiri katika wosia.

Wosia ni tamko au maandishi anayotoa mtu wakati wa uhai wake akieleza mgawo wa mali zake kwa warithi wake baada ya kifo chake. Kwa sheria zetu, wosia unapaswa kuwa siri. Shujaa mwanamke huyu aliacha wosia wa wazi, hivyo hakukuwapo mgogoro wowote.

Kuna aina kuu tatu za wosia. Wosia wa maandishi, wosia wa mdomo/matamshi na wosia wa wakfu. Kwa walio wengi, wosia wa mdomo na maandishi ndio maarufu sana. Wosia wa wakfu ni kwa matajiri ambao hukabidhi mali zao kwa wakfu, kisha warithi wakaendelea kutunzwa maisha yao yote.

Taratibu za kutoa wosia au kuandika wosia zinatofautiana kulingana na mila, desturi, dini au sheria ya mirathi inayotumika. Kwa Tanzania, wosia unaandikwa kisheria ama kwa kutumia Sheria za Kimila (The Local Customary Law (Declaration|) No. 4 Order 1963 au Sheria za Kiserikali zilizorithiwa kutoka kwa Waingereza (The Indian Succession Act ) iliyopitishwa India mwaka 1865 na sisi kuirithi vivyo hivyo ilivyo.

Sheria nyingine inayotumika katika mirathi ni Sheria za Kiislamu. Mtoa wosia anaruhusiwa kurithisha theluthi moja ya mali yake kwa mtu yeyote na theluthi mbili ni lazima zirithiwe na warithi halali.

Masharti ya kutoa wosia, ni mtoa wosia lazima awe na akili timamu, awe ametimiza miaka 18 na kuendelea, aonyeshe tarehe, mwezi na mwaka ulioandikwa na majina ya warithi. Mtoa wosia ahusishe mali zake binafsi na si za mtu mwingine. Wosia ni siri ya wanufaika hawatakiwi kuujua, ushuhudiwe na mashahidi wawili, kwa mtoa wosia anayejua kusoma na kuandika na kwa yule asiyejua kusoma au kuandika.

Mashuhuda wake lazima wawe wanne na wajue kusoma na kuandika. Mtoa wosia lazima aweke saini yake na kama hajui kusoma na kuandika aweke alama ya dole gumba la mkono wa kulia. Mashuhuda lazima waweke saini zao tena kwa wakati mmoja.

Pamoja na maelezo hayo, mada yangu ya leo inajikita katika kipengele kimoja tu cha wosia, kile cha usiri. Kwa maoni yangu, huu usiri katika kutoa wosia ndicho chanzo kikuu cha migogoro yote ya mirathi na dhuluma yote ndiko inakotokea.

Naendesha somo hili kutokana na yule shujaa wetu mwanamke niliyemzungumza wiki iliyopita, si tuu alikikubali kifo, bali baada ya kujaliwa umri wa mrefu wa miaka 85, aliwaheshimu baba yake na mama yeke, hivyo kupata miaka mingi na heri duniani. Miongoni mwa heri hizo ni kujaaliwa heri ya kuacha wosia wa wazi. Hivyo na sisi wote tuliopo duniani hivi sasa, kila mmoja ana wazazi, siku zote tujitahidi kwa kadri ya uwezo wetu, "Tuwaheshimu baba na mama, tupate miaka mingi na heri duniani".

Shujaa wetu, mwanamke huyu, alizaliwa katika familia ya watoto wanane, baba yao alifariki dunia siku nyingi, hivyo walibaki na mama yao. Yeye alipostaafu serikalini na kurudi kijijini, alimchukua mama yake na kuishi naye hadi kifo kilipomkuta. Hivyo na yeye, baada ya kutimizi umri wa miaka 80, alimkaribisha mtoto wake wa kike, kuishi naye mpaka kifo kilipomkuta.

Jambo la muhimu alilofanya ni kujiandaa kwa kifo, ikiwemo kwanza kuandaa wosia wa mdomo na kumweleza kaka yake mkubwa. Baada ya hapo alituita watoto wake wote na kutueleza kuwa ameisha gawa mali zake zote likiwemo shamba lake, hivyo ikitokea siku yeye hayupo, huyo kaka yake atawapa wosia wake. Mwanzo wosia huu ulikuwa siri.

Licha ya kutoa wosia wa kauli kwa kaka yake, siku ya siku akaita tena watoto wake wote, akaelekeza ichukuliwe kalamu na karatasi na kutoa wosia wa wazi na huku mtu akiandika kila kitu, iwapo kuna jambo litamtokea huyo kaka yake. Amini usiamini, Januari 2, 2022, huyo kaka yake alifariki dunia na kuzikwa Januari 5. Mwezi mmoja baadaye, yaani Februari 2, 2022 huyu shujaa wetu na yeye aliitwa mbinguni tarehe ile ile na kuzikwa tarehe ile ya mwezi uliofuata huku akiwa ameacha ule wosia wa wazi wa maandishi.

Uwapo wa wosia wa wazi wa maandishi, ulioandikwa kwa uwazi, huku warithi wote wakisikia, si tu unaepusha migogoro bali pia unaondoa sononeko la mioyoni la warithi kutotendewa haki kwa sababu warithi wote mnakuwa mlisikia wosia ukitamkwa, hivyo wote kuheshimu wosia wa marehemu.

Kwa vile sheria zetu tumezirithi kwa Waingereza zikitokea India, tumerithi kila kitu kama kilivyo 'para material' (neno kwa neno), tufike mahali tuachane na baadhi ya vipengele vinavyosababisha migororo, kikiwemo hiki kipengele cha usiri. Iwe chaguo la mtu anayetaka kuandika wosia, awe huru kuchagua, wosia wa siri au wosia wa wazi. Kwa kilichotokea juzi pale kijijini Kirua Vunjo, Moshi, baada ya msiba wa shujaa huyu, natamani kitokee Tanzania nzima. Kama kila mwenye mali atakuwa wazi kwa warithi wake, naamini faida za uwazi katika mirathi zina maslahi makubwa zaidi kuliko usiri.

**RIP Shujaa Mwanamke Yule. Wasalaam.**

**+255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Nyie viongozi msimchoshe Chifu Hangaya wetu



Na Joseph Kulangwa

**Rais anapoteua kiongozi wa kwenda kumwakilisha wilayani na mikoani, hutarajia kumwona akitimiza wajibu wake kwa nafasi ile ile ya Rais aliyemteua badala ya kumsubiri.**

HUWA nakaa nafikiria, mathalan una wanao wakubwa wana vyumba vyao, umewanunulia samani zote kuanzia vitanda, magodoro na viti na kuwaambia wavitunze viwatunze.

Lakini unafanya hivyo ukijua fika kuwa vikiharibika mambo yote yanakuwa mikononi mwako kuvirekebisha na hata kununua vingine ukilazimika kwa kuwa tu wewe ni mzazi.

Na hata anapoingia mdudu katika vyumba hivyo, watoto hao huwa na wajibu wa kuhakikisha anaondoshwa ili kulinda maisha yao na ya mtu yeyote atakayethubutu kuingia chumbani.

Kwa kifupi, haitamsubiri baba au mama kuingia katika vyumba hivyo kukagua samani na kupambana na mdudu aliyeingia chumbani kwa kuwa aliye karibu na samani na mdudu huyo ni atumiaye chumba hicho.

Hailazimiki kumsubiri mama au baba kufanya yote hayo huku mtoto una uwezo wa kufanya hivyo hadi inaposhindikana ndipo mmoja au wazazi wote wawili watakapoingia kudhibiti hali hiyo.

Hii naisema kwa kuangalia viongozi wetu nchini wanavyotenda na kutimiza wajibu wao hasa wanapokuwa wamepewa majukumu na mamlaka za uteuzi kuzifanya.

Rais anapoteua kiongozi wa kwenda kumwakilisha wilayani na mikoani, hutarajia kumwona akitimiza wajibu wake kwa nafasi ile ile ya Rais aliyemteua badala ya kumsubiri.

Wewe ni Mkuu wa Mkoa mathalan, au ni Mkuu wa Wilaya, umepewa jukumu la kusimamia mkoa au wilaya, unaapa kisha unaingia ofisini unakwenda kukaa huko tu ukisoma magazeti na kusogoa.

Unafanya hivi huku wananchi wako wakipiga miayo na kulia njaa kwa kutokuona wewe ukiwazungukia kukabiliana na matatizo yao na kuwaletea maendeleo.

Unasubiri mpaka aje Rais, aonyeshwe mabango ndipo ajue kuwa katika wilaya au mkoa huu kuna mtatizo haya au yale, hiyo si kumtendea haki aliyekuteua na unastahili kuacha kazi hiyo afanye mwingine.

Hayo tunayashuhudia leo tunamwona Chifu Hangaya akihangaika na nchi hii kuzunguka huku na huko na kukutana na masahibu mengi mengi ya wananchi yasiyofanyiwa kazi.

Anajikuta Chifu akitumbua watu akiwa njiani kwa kusikia kuwa mahali fulani wateule fulani hawakufanya anavyotaka katika kuwaletea maendeleo wananchi, wamefakamia fedha zote zikiwamo za UVIKO-19.

Hivi mtu kama huyu akiamua kula sahani moja na ninyi wezi mtamlaumu kweli? Atakuwa mtu wa aina gani akuvumilie wewe baada ya kukuamini kuwa anakupa madaraka umsaidie, lakini wewe unamsukumiza!

Rais anafika mahali anakuta mradi umesimama kwa miaka nenda rudi, eti kwa sababu kuna viongozi wanabishana huku kule, huyu anavutia huku na yule anavutia kwake ili mradi kuonyeshana misuli, kweli?

Kiongozi Mkuu wa nchi anapita mahali anakuta kuna mashimo na mahandaki barabarani, msimamizi anajionea ni sawa tu, hasemi kitu mpaka Rais anafika na kukuta madudu hayo, halafu akuache tu!

Mwishoni mwa mwaka jana tu hapa, maji yakapungua Mto Ruvu tukahofia hata Jiji la Dar es Salaam kukumbwa na ukame wa maji kwenye mabomba. Ilipofuatiliwa ikabainika kuwa kumbe kuna mifugo inayabugia kila siku ya Mungu.

Unajiuliza hivi wakati wote huo wasimamizi wa Mto huo walikuwa wapi mpaka kusubiri Waziri Mkuu au Rais afike ndipo atoe tamko la kutaka wasimamizi kusimamia maji ya Mto huo na kunyima vibali vya mwekezaji.

Kwa kufikiria haraka haraka, hivi kweli wasimamizi walikuwa hawaoni mwekezaji amevamia Mto na kunyweshea mashamba yake na kupunguza maji mtoni? Hivi kweli hapakuwa na mtu kuona wafugaji wakinyweshea mifugo?

Unashangaa siku nyingine, unasikia kiongozi fulani kaenda mahali fulani kufungua kitu fulani, lakini kufika anakataa kukifungua kwa sababu hakina ubora, hakina viwango fulani.

Wakati unashangaa, unajiuliza hivi hapakuwa na kiongozi wa chini kubaini kwamba darasa hili si la kiwango au zahanati hii, si ya kiwango na hivyo kukataa kabla ya kumsubua tuseme Waziri Mkuu kutoka huko aliko kwenda kushughulikia jengo zombi?

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Wananchi Ngorongoro wasikilizwe, wasihamishwe kwa nguvu ya mitutu



Na Thobias Mwanakatwe

MAMLAKA ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) ambayo inapatikana Mkoa wa Arusha ilianzishwa mwaka 1959, ilipofika Aprili 17, 2018 ikatambuliwa rasmi na Umoja wa Mataifa kupitia shirika lake la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kuwa hifadhi jiolojia ya Ngorongoro Lengai.

Sifa kuu mamlaka hii ambayo huwezi kuikuta mahali popote duniani ni kwamba ni eneo ambalo ni hifadhi mseto. Kuna viumbe hai aina tatu wanaoishi kwa pamoja ambavyo ni watu ambao zaidi ni jamii ya kabila la Wamaasai, mifugo yao kama kondoo, mbuzi na ng'ombe na wanyamapori.

Wakati wa kuanzisha hifadhi hii, kulikuwa na malengo makuu matatu ambayo ni, kulinda maslahi ya jamii kabila la Wamaasai ambao wameishi na wanyamapori kwa miaka mingi pasipo uharibifu wowote ule. Jamii ya kabila la Wamaasai inachukuliwa kuwa wahifadhi asili kwa sababu ya kuishi na wanyamapori kwa muda mrefu kihistoria. Wamekuwa walinzi wazuri wa wanyamapori na kivutio kikubwa cha watalii wanaofika kwenye hifadhi hiyo.

Malengo mengine ya kuanzishwa kwa mamlaka hiyo yalikuwa kuendeleza uhifadhi na utalii mambo ambayo tangu kuanzishwa kwake, yamekuwa yakizingatiwa na jamii ya Wamasai, hivyo kuifanya hifadhi hiyo kuzidi kuwa kivutio kikuu cha utalii kupendwa na watalii wanaotoka mataifa mbalimbali.

Nimeanza na utangulizi huo kutokana na kampeni kali inayofanywa hivi sasa na baadhi ya vyombo vya habari kutaka wafugaji jamii ya Kimasai waondolewe ndani ya hifadhi kwa madai kuwa wanafanya uharibifu na kuhatarisha hifadhi kutoweka. Kampeni ya kutaka Wamasai waondolewe ambayo inaendeshwa na baadhi ya taasisi zisizo za kiserikari kwa kuvishirikisha vyombo vya habari, imeanza kwa kasi Januari, mwaka huu, haijafahamika kilicho nyuma ya pazia ya jambo hili.

Nikisoma kwenye mitandao ya kijamii na hata baadhi ya vyombo vya habari kampeni hiyo inavyoendesha nimekuwa na maswali mengi yasiyo na majibu. Baadhi ya maswali ninayojiuliza, nina imani kwamba na wengine wanajiuliza ni kwamba je, jamii ya Wamasai wamekuwapo ndani ya hifadhi hiyo kwa miaka mingapi, wamepita viongozi wa mamlaka wangapi hawakuwahi kuja na hoja ya kutaka waondolewe, kwa nini leo kampeni imeshika kasi na kutumia fedha za umma. Pia najiuliza kwa nini jambo hili la kutaka kuwaondoa limekuja baada tu ya uchaguzi mdogo wa ubunge katika jimbo la Ngorongoro uliofanyika Desemba 11, 2021?

Sitaki kujiingiza kisiasa, lakini kwa kukumbushana tu wakati wa kampeni za uchaguzi huo mdogo, Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, alitua Ngorongoro na kufanya mkutano mkubwa wa kampeni na kuzungumza na mamia ya wananchi wa tarafa ya Ngorongoro.

Katika mkutano huo, Pinda aliwaondoa hofu wananchi wa tarafa ya Ngorongoro kuhusu tetesi za kuondolewa katika eneo la NCAA. Katika mkutano huo uliofanyika katika kata ya Nainokanoka, aliwaambia wananchi hao kuwa wawe watulivu kwa sababu suala la kuondolewa katika eneo hilo limeshawasilishwa serikalini na wazee wa mila.

Kiongozi huyo aliongeza kuwa ana imani mkubwa hoja ambayo pia yanaelekeza changamoto za wananchi wa tarafa ya Ngorongoro zijadiliwe kuanzia ngazi ya kitongoji, yafanyiwe kazi na serikali.

Mapendekezo haya yalitokana na agizo alilolitoa Rais Samia Suluhu Samia wakati anahutubia wananchi wa mkoa wa Arusha katika uwanja wa Sheikh Amir Abeid Oktoba 17, 2021. alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, kukutana na malaigwanani kuzungumza nao na mapendekezo watakayoyatoa yawasilishwe kwake.

Ukisoma na kusikiliza alichokisema Pinda na hii kampeni inayoendeshwa kutaka kuwaondoa jamii ya Wamasai, unazidi kujiuliza maswali yasiyo na majibu maana tangu kauli hiyo itolewe, takribani miwili imepita. Je, nini kiko nyuma ya pazia katika suala hili?

Tamko la Pinda liliwavutia na kuwatia moyo wafugaji wa Kimasai walioko eneo la hifadhi hiyo lakini baada ya uchaguzi kwa nini waanze kusononeshwa kwa kampeni hii inayoendelea? Nani kawatuma wanaoendesha kampeni hii kutaka waondolewe na amelipwa shilingi ngapi?

Aidha, kwa nini wahusika ndani ya serikali na mamlaka wamekaa kimya, hawataki kutoa tamko? Au wanataka kuwaaminisha wananchi kuwa haya yanayofanyika yana baraka za viongozi? Ukizungumza na jamii ya Wamasai (wafugaji) wanasema hawana tatizo na serikali wala chama tawala bali wanachotaka wakae meza moja kujadili jambo hilo na kulipatia ufumbuzi badala ya kuendesha kampeni za kutaka kuwaondoa kinguvu kwa mitutu.

Wanasema hoja kwamba wafugaji wamekuwa wengi eneo la hifadhi si ya msingi. Wanahoji kwamba siku Watanzania wakiwa wengi ndani ya nchi yao wataondolewa na kupelekwa nchi nyingine kwa kuwa wamekuwa wengi?

Wanaongeza kuwa mambo yanayofanywa na viongozi wa NCAA ni kuzidi kuongeza chuki dhidi ya wafugaji kwa kuwa yako mambo mengi yanafanywa pasipo hata kuwajulisha wenyeji. Kifupi wenyeji (jamii ya wafugaji wa Kimasai) ambao kwa muda mrefu wamekuwa walinzi wa hifadhi hii, leo wanaonekana maadui.

Jambo kubwa wanalojiuliza ni kwa nini kampeni hii imekuja hata kabla majibu hayajatoka kuhusu sakata la chumvi 'feki' iliyozua mjadala mkubwa wafugaji ambayo waligawiwa na NCAA na baadaye kubainika haikuwa na viwango kwa kuwa ilichanganywa na mawe ambayo yanaweza kuleta athari kwa mifugo?

Ukiangalia nembo ya NCAA inajieleza jinsi ambavyo wenyeji ambao ni wafugaji wa jamii ya kimasai walivyo na mchango katika kulinda hifadhi hii. Lakini kwa nini leo wanaonekana maadui na sasa kampeni inafanyika kutaka kuwaondoa.

Nadhani viongozi wa mamlaka waendeshe shughuli zao kwa kusimamia malengo yote matatu yaliyosababisha kuanzishwa kwa hifadhi hiyo. Suala la kutaka kuwaondoa wafugaji wa jamii ya wafugaji ndani ya hifadhi lisitishwe na lisifanywe kwa shinikizo la baadhi ya watu wenye maslahi yao. Itafutwe njia nzuri ya kukaa meza moja kujadili suala hili na kulipatia ufumbuzi.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**

## DARASA LA NDOA

# KUISHI MBALI BAINA YA WENZA KUNAVYOATHIRI NDOA, FAMILIA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

ILI kuleta tija mahali pa kazi, watu ni rasilimali muhimu. Hakuna taasisi, shirika, kampuni au serikali inayoweza kufanya kazi bila kuwa na rasilimali watu. Kwa mantiki hiyo, taasisi zimeundwa na zinafanya kazi zake kupitia watu. Mafanikio yoyote mahali pa kazi yanategemea watu, hivyo watu ni chachu ya mafanikio katika maeneo ya kazi.

Kutokana na ukweli huo, waajiri makini huwekeza katika rasilimali watu kwa kuwajengea uwezo na kuhakikisha watumishi wana furaha mahali pa kazi. Ni vigumu mtumishi asiye na furaha kutoa huduma bora. Siku zote furaha inapokosekana kwa mtumishi huathiri utendaji wake wa kazi na kupunguza uzalishaji, huondoa hali ya kujithamini (personal value), kujiamini (confidence), huvuruga uhusiano wake na watu wengine; hukosa hamasa (motivation) na kusababisha hasara mahali pa kazi.

Upangaji wa vituo vya kazi na uhamisho wa watumishi usiojali ustawi wa familia, huchangia kuondosha furaha ya mtumishi mahali pa kazi. Kwa muktadha wa makala hii, familia maana yake ni baba, mama na watoto.

Katika miaka ya karibuni, tumeshuhudia ongezeko la watumishi wanandoa wanaoishi mbali na familia zao. Kwa mfano, kituo cha kazi cha mume kiko Pwani huku kituo cha mke kikiwa Kigoma au mume anaishi Njombe na mke anaishi Arusha. Kwa namna yoyote ile, umbali wa jinsi hii hauwezi kuiacha familia salama.

Kitendo cha mume au mke kuishi mbali na mwenzi wake ni changamoto kubwa nzito. Mara nyingi, hali hii imesababisha vishawishi na kuathiri uhusiano wa wanandoa wengi kwa sababu ya matatizo yanayotokana na umbali. Umbali na hali ya upweke vimechochea baadhi ya wanandoa kuanzisha uhusiano mpya nje ya ndoa kwa kile kinachoelezwa kuwa ni kufidia pengo la umbali. Kwa ujumla, waathirika wakubwa katika hali hii ni wanawake na watoto. Uhusiano huu ukiishakolea na kuota mizizi, husababisha wanandoa kupoteza mvuto na thamani ya mwenzi wake. Hali hii hutengeneza mazingira ya migogoro isiyo ya lazima katika ndoa. Baadhi ya ndoa zimebaki kuwa za heshima tu na kupoteza uhalisia wake. Athari zake ni kubwa kwa wanandoa wenyewe na watoto waliozaliwa katika ndoa hizo.

Wako wanandoa ambao wamevurugwa, wamejeruhiwa nafsi na ndoa kuvunjika kwa sababu ya kuishi mbali na wenzi wao. Wanandoa wanapoishi huku na kule, huongeza gharama za maisha, hali ambayo huathiri tabia na mienendo yao. Umbali husababisha msongo wa mawazo ambao huathiri afya ya akili na mwili, hupunguza kiwango cha mshikamano wa wanandoa, mvuto, upendo na joto la ndoa.

Mume na mke wanapoishi mbalimbali huathiri watoto kisaikolojia na kimakuzi kwa sababu ya kukosa malezi ya wazazi wote wawili. Wako watoto ambao wamewachukia wazazi wao na kupoteza mvuto wa baba au mama au wote kwa pamoja kwa sababu ya kuhisi kutokupendwa, kupuuzwa na kutelekezwa. Malezi mabaya ya watoto huchangia mmomonyoko wa maadili katika jamii.

Utumishi ni popote na kwamba mazingira ya kikazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za kazi hulazimu mume au mke kuishi mbali na familia yake. Hata hivyo, kuna umuhimu mkubwa kutafakari kwa makini na kulipa uzito unaostahili suala hili kwa kuzingatia kuwa wako watumishi wanandoa waliopangwa vituo vya kazi lakini hawana furaha ya kazi na maisha. Ufanisi wa utendaji wao wa kazi umeshuka na kuleta athari mahali pa kazi. Hali hii hujitokeza kwa kuwa mtumishi anatumia muda wake mwingi zaidi kufikiri kuhusu familia na matatizo ya nyumbani kwake kuliko kazi.

Kwa kuzingatia mazingira halisi wanayokutana nayo, baadhi ya watumishi wanandoa wanaoishi mbali na familia zao, natoa ushauri kwa serikali kuchukua hatua za makusudi ili kurekebisha hali iliyopo sasa. Ni muhimu zitungwe sheria na kanuni zenye lengo la kuweka utaratibu mzuri zaidi utakaolinda ndoa na ustawi wa familia kwa madhumuni ya kuongeza tija na ufanisi kazini.

Ndoa ni kitovu na msingi wa familia, jamii, taifa na maendeleo. Msingi wa ndoa ukiyumba, kila kitu kitayumba. Kazi zitayumba, ustawi wa familia utayumba, jamii itayumba, taifa litayumba, na maendeleo yatayumba kwa sababu ya kukosekana kwa nguvu kazi yenye utulivu na amani. Furaha na amani ya mtumishi ni chachu ya mafanikio mahali pa kazi na maendeleo ya Taifa.

Mungu alianzisha ndoa ili mume na mke waishi pamoja kwa furaha. Mafanikio na baraka katika kazi zetu huanzia nyumbani. Mafanikio na baraka hizi hudhihirika pale ndoa zinapokuwa imara. Nyumbani kukiwa vizuri, kuna uwezekano mkubwa kazini kukawa vizuri pia. Kazi zipo ili kuleta furaha na siyo kuleta upweke na maumivu. Kwa mantiki hiyo, kazi zisiondoe utu na thamani ya familia.

**Mungu ibariki Tanzania!**

**●Dk. Mlyuka ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

FEBRUARI 13, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 14


## Katlesi ya nyama kiburudisho tosha



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Namna ya kupamba chumba siku ya Valentine




## KATUNIKA

Ukurasa 16




# VALENTINE DAY

## Mavazi yanayoonyesha mapenzi mazito

Ukurasa 13


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | K | W | E | T | U |
| ■ | W | ■ | ■ | W | ■ |
| B | E | I | ■ | A | ■ |
| ■ | N | ■ | A | N | A |
| ■ | Y | ■ | ■ | G | ■ |
| T | E | N | G | A | ■ |

## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | | | | | |
| ■ | | ■ | ■ | | ■ |
| | | | ■ | | ■ |
| ■ | | ■ | | | |
| ■ | | ■ | ■ | | ■ |
| | | | | | ■ |

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
UZI, DAU, TANGA, TINGA, GAWANA, TAZAMA

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Grace alikuwa na bibi yake akisukwa nywele kwa ajili ya maandalizi ya kwenda shuleni kesho yake.

Wakati akiendelea kusukwa bibi yake alikuwa akiimba nyimbo mbalimbali ambazo zilimuhamasisha kusuka kwa haraka na umakini mkubwa. Grace aligeuza kichwa chake na kumuuliza bibi yake.

Grace: Bibi mbona wakati wote unaimba nyimbo, tena za zamani?

Bibi: Mwanangu wahenga walisema 'Ya kale ni dhahabu'

Grace: Unamaanisha mambo ya zamani yalikuwa kama dhahabu?

Bibi: Ndiyo mjukuu wangu yaani mambo mazuri ya zamani yanaendelea kuishi tofauti na sasa hivi.

**SWALI**

Nyegere ni mnyama anayejulikana kwa sifa zipi?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Magumu unayopitia kimaisha yamesababishwa

KARIBU tena msomaji tuendelee na mada yetu ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Leo nitazame baadhi ya ujumbe kutoka kwa wasomaji wa safu hii wakitaka msaada wa jinsi wanavyoweza kuondokana na mambo magumu wanayokabiliana nayo kimaisha.

Siku zote kuna matatizo yanayoweza kusababishwa na watu wa ndani au nje ya familia. Mara nyingi, familia inapopatwa na tatizo, lazima kidole kitanyooshewa zaidi mtu wa nje, awe ni jirani au hata rafiki.

Ni mara chache sana atatajwa mtu wa ndani ya familia husika, tena kwa kumshuku tu na siyo kwa kuamini. Kumbe umdhaniaye siye, aweza kuwa ndiye. Na neno la Mungu linasema, adui wa mtu ni wa nyumbani mwake.

Yuko baba mmoja alikuwa na kazi yake nzuri, biashara zikienda vema lakini ghafla afya yake ikaanza kuzorota. Akajikuta anaanza kukataa chakula, hataki kuoga wala kupiga mswaki.

Hataki kutoka nje ya nyumba yake anajifungia ndani. Anakimbia watoto wake, mke na hata ndugu zake. Ni takriban miezi sita sasa akipambana na hali hiyo. Jamaa zake na hata wazazi wake wakamkatia tamaa.

Ndipo likamjia wazo atafute simu za watumishi wa Mungu kwenye mitandao aweze kupata msaada wa maombi. Akabahatika kupata namba ya mtumishi mmoja wa Mungu akamuomba amuombee aondokane na yale anayopitia.

Baada ya kumsimulia yanayomsibu, yule mtumishi ikabidi amfuatilie hadi nyumbani kwake ambako alifika na kumuombea. Baada ya maombi, mtumishi akamwambia anyanyuke kwenye kiti amfuate nje.

Ndipo kwa kuamini akanyanyuka na kweli akatembea mwenyewe kwenda nje pasipo kushikiliwa na mtu. Hatua ya pili, akaambiwa achukue mswaki asafishe kinywa, jambo ambalo aliweza. Kabla ya hapo aliuogopa mswaki eti akiuingiza kinywani ataumeza!

Ndani ya wiki moja mgonjwa huyu akaweza kufanya mambo ambayo hakuweza kwa miezi sita aliyokaa ndani. Aliweza kupanda daladala mwenyewe kwenda kwenye maombezi. Lakini cha ajabu, familia yake badala ya kufurahia maendeleo mazuri ya ndugu yao, wakamchukua kutoka mjini alikokuwa na kumrudisha kijijini kwao.

Swali la kujiuliza; mbona katika miezi hiyo sita aliyokaa ndani hakupelekwa nyumbani kwa msaada zaidi? Kuombewa na kupata nafuu kwanini familia isione ni kwa neema ya Mungu? Vipo vyanzo vya matatizo kwenye familia vinajulikana lakini vinafumbiwa macho!

Lakini ni vema tukafahamu kuwa Mungu anaona yote yaliyojificha kwani anasema, "Mambo ya siri ni ya BWANA, Mungu wetu; lakini mambo yaliyofunuliwa ni yetu na watoto wetu".

Msomaji mwingine akatuma ujumbe ufuatao; - naitwa Anthony umri miaka 26, mwenyeji wa Dodoma, kwa sasa nipo Zanzibar. Moja ya makala zako imenigusa nahisi nimefungwa. Ni takribani miaka saba mambo hayaendi nahisi kuna kitu siyo bure.

Nilianza kuona tofauti nilipomaliza kidato cha nne. Nilifanikiwa kupata divisheni I. Cha ajabu nilipoanza tu kidato cha tano nikawa nasoma PCM vizuri tu. Ila nikikaribia mitihani wiki moja kabla, nashikwa na ugonjwa wa ajabu, nashindwa kusoma kabisa hata kufanya mtihani wenyewe.

Ikasababisha kutofanya vizuri katika mitihani, nikachukua diploma ya udaktari. Nilidhani ilikuwa ni hali ya A Level tu na bahati haikuwa yangu. Lakini hata nilipoingia chuo ngazi ya diploma, hali ilikuwa vile vile, nikakata tamaa sana.

Nikajitahidi, bahati nzuri nikafaulu kawaida ingawa uwezo wa kufaulu viwango vya juu nilikuwa nao. Kimbembe kikaja kwenye kazi. Nahangaika tu, kila kazi nitakayopata nafanya vizuri ila nanyonywa na kipato ninachoingiza ni kidogo, nacho hakikai.

Sijui kinaenda wapi kwani najitahidi kujibana, nitunze pesa ili niendelee kusoma lakini hazikai. Mipango ninayo mizuri, fursa yoyote nzuri ikitokea nakubalika lakini kinatokea kitu naumwa nayo fursa inapotea, naikosa!

Hayo ndiyo yamekuwa maisha yangu. Naona kwa staili hii sifiki. Kwenye makala yako kila ulichosema, mimi ninacho. Nina malengo mengi sana lakini sioni chochote mbele yangu kwa sasa. Naomba unisaidie.

***Hivyo ndivyo anavyomaliza ujumbe wake msomaji wetu. Hakika anapitia magumu na mazito lakini kwa Mungu yote yanawezekana. Wiki ijayo nitachambua baadhi ya visababishi vinavyofanya kijana Anthony apitie hayo yote. Je, una maoni, ushauri? Tuma ujumbe 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Serikali ichukulie kwa umakini 'maswali ya kudumu' ya wabunge

KILA siku kunapokuwa na vikao vya bunge, wabunge wanapata kuuliza maswali ya msingi ambayo hufuatiwa na maswali ya nyongeza. Wote huuliza mambo yanayogusa majimbo yao ambayo mengi hujikita kwenye maji, barabara, afya na elimu.

Tangu mkutano wa sita wa bunge la 12 uanze Februari, mwaka huu, wabunge wameongoza kwa kuuliza maswali Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Kila mawaziri wanapojibu maswali ya msingi, wabunge wengi husimama kuuliza maswali ya nyongeza na hata waziri anapomaliza kujibu wengi hunyanyuka kutaka kuuliza. Wabunge wengi wanakumbushia ahadi za marais tofauti tangu awamu ya nne, Jakaya Kikwete, awamu ya tano, Hayati John Magufuli na awamu ya sita, Samia Suluhu Hassan.

Wengi huonyesha uzito kwa kueleza kuwa barabara hiyo imeahidiwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi kuwa itajengwa, hivyo wanaitaka serikali kueleza ni lini ujenzi utaanza.

Wawakilishi hao wa wananchi huuliza ni lini serikali itajenga barabara fulani ambayo ni ahadi ya fulani au imekaa muda mrefu bila kujengwa au ni barabara muhimu kwa uchumi wa eneo fulani.

Wengi hujitahidi kueleza umuhimu wa barabara hizo kiuchumi na kwa maendeleo ya wananchi lakini majibu mengi ya serikali huwa ni kuwa "fedha zinatafutwa, upembuzi ya kinifu unafanyika, tuko kwenye mchakato".

Pia wako wabunge huyarudia maswali yale katika vipindi tofauti vya bunge na majibu huwa yale yale au yamebadilishwa kidogo lakini hayatoi suluhisho la kudumu.

Kwa TAMISEMI kilio kikubwa ni barabara za vijijini ambazo kila siku wabunge kadhaa huzilizia kiasi cha Spika Dk. Tulia Ackson, kueleza serikali kufanya tathmini ya barabara zote zilizoharibika na itoe maagizo kwa Wakala wa Barabara Vijijini (TARURA) kuchukua hatua.

Katika mjadala wa bunge walishauri serikali kurudisha Tume ya Mipango ambayo itaangalia barabara za kimkakati zijengwe na kukamilika kabisa kuliko kujenga kilomita nne kwa kila jimbo ili kuwaridhisha wabunge na wananchi.

Baadhi ya wabunge wamegeuka kuwa walalamikaji au kutaka kuelezwa lini barabara hiyo itajengwa, jambo ambalo wakati mwingine haliisaidii serikali juu ya hatua gani ya kufuata.

Eneo lingine ambalo linaulizwa ni huduma za afya hasa upatikanaji wa dawa na bima ya afya lakini kwa sasa serikali imeahidi kuleta bungeni Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, ili kuwezesha watu wote kupata bima.

Kwa ujumla ni lazima mambo ya msingi kama barabara yakaangaliwa kwa jicho la pekee kwa kuwa ni muhimu kwa maisha ya watu.

Naipongeza serikali kwa kuunganisha mikoa kwa barabara za lami na sasa kazi kubwa ni kuunganisha wilaya kwa wilaya, tarafa kwa tarafa, kata kwa kata, kijiji kwa kijiji, mtaa kwa mtaa au kitongoji kwa kitongoji.

Ikiwa itafika mahali kila mahali kukawa na miundombinu ya barabara, maana yake huduma za maendeleo zitawafikia wananchi kwa urahisi zaidi. Wananchi wataweza kusafirisha bidhaa na mazao kutoka eneo moja hadi lingine kwa urahisi zaidi.

Hali hii inaonyesha kuwa kuna kazi kubwa ya kufanya kujenga miundombinu ya barabara, ili kuondoa kero hii ifike wakati mbunge akisimama anachangia masuala mengine.

Kwa ujumla, hadi sasa licha ya jitihada nyingi zilizofanyika na zinazofanyika, bado kilio cha mahitaji ya msingi ni kikubwa ndiyo maana ni muhimu kuhakikisha kodi au fedha ya umma inatumika vizuri.

Siku zote kupanga ni kuchagua, hivyo ni lazima kuangalia tunataka nini kwa sasa ili kama inawezekana barabara za kimkakati zikamilike huku zingine zikiendelea kujengwa kidogo kidogo kila mwaka.


Nafahamu barabara ya Mwanga hadi Mwaniko na Usangi wilayani Mwanga, ambayo bado inajengwa kila mwaka kwa fedha kilomita mbili, sasa kwa miaka 10 inaendelea kujengwa jambo ambalo limekuwa kero na usumbufu kubwa wakati mwingine kutumia fedha zaidi kwa kuwa maeneo yaliyojengwa muda mrefu yanahitaji ukarabati.

Iko faida ya kujenga kidogo kidogo kwa kuwa keki ya taifa inagawanywa kwa wote lakini ziko barabara kwa zaidi ya miaka 20 bado hazijaanza na wala hazimo kwenye mpango licha ya kuwa ni ahadi ya Rais.



NGUO zilizotengenezwa Kiafrika zinapendeza zaidi kuvaliwa kwa maharusi siku ya kufunga ndoa. Pichani ni baadhi ya mavazi ya harusi yaliyoegemea mazingira ya Kiafrika.







# MITINDO

Na Christina Mwakangale

# VALENTINE DAY
# Mavazi yanayoonyesha mapenzi mazito




KESHO ni siku maalumu kwa watu wanaopendana, ni wakati wa watu kutafakari na kuonyesha wazi upendo wao wa dhadi kwa watu wao wa karibu.

Siku hii ambayo inaadhimishwa kila mwaka, vazi la rangi nyekundu ndilo hutawala kila mahali, hii ni kuonyesha wazi kwamba raha ya upendo, kujali na kuthamini ipo katika mioyo yao.

Wabunifu wanafanya kazi ya ziada kutengeneza nguo zenye mitindo ya kupendeza bila shaka kila mtu atataka kuonekana vizuri zaidi pale anapotoka katika matembezi ya mchana au jioni.

AINA YA NGUO

Kuchagua ni nguo gani inafaa kwa ajili yako, hiyo itatokana na utashi wako binafsi, lakini usiende kinyume na rangi husika ya siku hiyo.

Unaweza kuvaa gauni la mikono mifupi au mirefu, koti au suruali za rangi nyekundu. Zote zinafaa kama zinalingana na mwili wako.

Unaweza kupendekeza kitu gani cha ziada unaweza kubeba, kama pochi au begi la mkononi na viatu vyote viwe vina rangi nyekundu.

Kumbuka kujiweka sawa kwa vipodozi murua ikiwamo rangi yako ya midomo ikiwa ni ile nyekundu na ikiwezekana hata rangi ya kucha.







UREMBO

**Na Mary Geofrey**

# VALENTINE DAY
## Furahia midomo inayosema



Wakati imebaki siku moja kuadhimisha siku ya Wapendanao maarufu kama 'Valentine Day' baadhi ya wanawake wanajiuliza watatokaje siku hiyo?

Lakini kwa wale wanaojua urembo, suala hilo ni dogo kwao kwani wanajua watatokaje wakiwa tofauti kuanzia mavazi hadi mwonekano wa sura.

Hata hivyo, muhimu hapa ni kuangalia utatokaje ukiwa na sura yenye midomo inayoashiria upendo, mahaba na upole.

Midomo yenye rangi nyekundu ni alama kubwa wakati wa siku kama hiyo, kwani huonyesha mapenzi ya dhati.

Wewe mwenyewe unaweza kujitengeneza uonekane una mvuto na kuongeza ushawishi katika mwonekano wako.

Ngozi ya midomo ni laini sana na inahitaji uangalizi wa hali ya juu kuhakikisha inakuwa katika hali hiyo siku nzima.

Kabla ya siku husika, anza matayarisho usiku kwa kutoa ngozi ngumu ya juu iliyokufa, unaweza kutumia mswaki wako baada ya kupiga mswaki pitisha kwa uangalifu kwenye midomo yako kisha paka Vaseline, mafuta ya mgando au lipshine.

Ni vizuri zoezi hili likafanyika usiku wakati ukijiandaa kulala itakufanya ukiamka uwe na midomo laini na yenye mvuto zaidi.

Kunywa maji mengi ya kutosha ili kufanya ngozi ya mwili wako na ya midomo kuwa laini na nyororo.

Siku ya pili unarudia tena, lakini badala ya kuweka lipshine, utapaka lipstick nyekundu kuzunguka midomo yako yote.

Dondoo za kufuata

Anza kwa kupaka kilainishi kabla ya kupaka rangi ya midomo.

Paka Lip Liner ya rangi inayofanana lipstick ambayo unatarajia kupaka.

Anza kupaka midomo ya chini ukifuatiwa na juu.

Kama unapendelea mng'ao zaidi unaweza kupaka lipshine kwa juu ili kung'arisha midomo yako.

Baada ya kufuata hatua hizo hapo, utakuwa umekamilisha upakaji mzuri wa Lipstick katika midomo yako na kuifanya ya kuvutia.



MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Katlesi ya nyama kiburudisho tosha

CHAKULA aina ya Katlesi ni kizuri kuliwa kama kiburudisho kutokana na ladha yake kuwa nzuri.

Hata hivyo, chakula hiki kinapendeza zaidi kama kikipikwa kwa nyama laini inayoiva haraka.

Hata hivyo, wengine wanapendelea kuweka kama chakula ambata na kingine kama wali au pilau.

Mahitaji

Viazi ulaya nusu kilo, chumvi, pilipili mbuzi moja, vitunguu saumu viwili, vitunguu maji viwili, karoti mbili na nyama au samaki nusu kilo.

Mahitaji megine ni unga wa ngano unaweza pia kutumia sembe robo kilo, mayai mawili, andaa nyama, osha na kata vipande vidogo.

Namna ya kuandaa

Andaa viungo, osha na kata vitunguu saumu na vitunguu maji na karoti, kata vipande vidogo. Ponda vitunguu saumu.

Weka viungo kwenye nyama, kitunguu saumu na chumvi.

Chemsha nyama na unaweza kuchemsha na pilipili ili kuipa harufu na ladha nzuri. Chemsha hadi maji yakauke kwenye nyama. Kama unatumia samaki utafanya vivyo hivyo.

Changanya nyama na viazi, unaweza pia kuweka nyama kati ya viazi. Kama unatumia samaki, unaweza kusaga samaki na kuchanganya na viazi ili kupata mchanganyiko sawia wa samaki na viazi.

Chukua kiazi chenye nyama au samaki chovya kwenye mayai halafu nyunyizia sembe au unaweza kuchovya pia.Weka kwenye mafuta jikoni ili kukaanga.

Vikiiva vizuri toa na weka pembeni. Unaweza kula mlo huu wakati wa asubuhi, mchana au jioni.



MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Boresha nyumba yako mara kwa mara

MABORESHO ya nyumba yanapaswa kufanyika mara kwa mara katika kuimarisha ustawi wake. Mbali na kufanya maboresho kwa ajili ya kuimarisha pia kunachangia kwa kiwango kikubwa iendelee kuwa na mvuto.

Leo nataka tuzungumzie namna ya kuboresha nyumba kwenye uso wake wa mbele.

Msanifu Majengo, Amos Kuvilo, anasema kuna umuhimu mkubwa wa kutofautisha uso wa mbele wa nyumba na maeneo mengine ya nyumba hiyo.

"Kuna nyumba zingine zimekosa mwonekano mzuri wa mbele na hivyo husababisha kushindwa kutofautisha uso wa mbele na wa nyuma wa nyumba au upande wa kulia na kushoto. Hapa ndipo tunasema kuna haja kwa msanifu kutumia maarifa kuandaa ramani ambayo itakidhi mahitaji ya nyumba husika,"anasema Kuvilo.

"Baadhi ya sehemu za mbele za uso wa nyumba ambazo ni muhimu kuzipendezesha ni nguzo ambayo ni sehemu ya jengo iwe ya duara, mstatili au mraba. Hii itategemea namna ilivyosanifiwa, lakini cha msingi ni kuhakikisha unatengenezwa kwa ustadi mkubwa," anasisitiza.

Pia anasema katika kutengeneza uso wa mbele wa nyumba ni vizuri kutumia malighafi ambayo ni rafiki kwa mvuto wa macho, imara na ambayo haina madhara kwa binadamu.

"Hili linawezekana kwa sababu Wasanifu wanafahamu malighafi bora za kutumia katika kutengeneza eneo hili kwa hiyo ni vema kuwatumia ili kuepuka madhara yasiyo ya lazima," anasema Kuvilo.

Mbali na nguzo, Kuvilo anasema madirisha nayo ni eneo muhimu ambalo linapaswa kuwekewa urembo hususani lililoko mbele ya uso wa nyumba.

"Na katika kutengeneza dirisha la mbele la uso wa nyumba, hapa napo kutategemea na vigezo vya sehemu au sababu za kisanifu, msanifu anatakiwa kutumia utaalamu wake kupendekeza aina ya dirisha kulingana na malighafi anayotaka kuweka iwe ni kwa mlalo au unyoofu," anasema.

Pia anasema eneo lingine la kuboresha kwenye uso wa nyumba ni milango ya nje.

"Milango ya nje bila kujali aina zake, hutumiwa kwa kuzingatia aina ya mtiririko wa kisanifu ili kutokupoteza mnyororo mzima wa mtindo na mpangilio wa jengo ulivyo," anabainisha.

Kuvilo anashuri kwamba wakati maboresho au matengenezo yanafanywa kwa ajili ya kupendezesha uso wa mbele wa nyumba, ni vema kutokusahau uchaguzi wa rangi kwenye ukuta na dizaini katika valanda lake katika uso huo wa mbele wa nyumba.



## Namna ya kupamba chumba siku ya Valentine



KESHO ni siku maalumu ya kuonyesha upendo na mapenzi kwa watu mbalimbali, na hata katika uhusiano ni wakati mzuri wa kutafakari ulipotoka, ulipo na unakokwenda.

Katika kukamilisha siku hiyo unaweza kuandaa chumba katika mwonekano tofauti kwa ajili ya mtu unayempenda ili mara anapofika anapata ujumbe kabla ya kufanya mazungumzo.

Kutokana na umhimu wake, hizi ni baadhi ya dondoo ambazo unaweza kutumia kupamba chumba chako kwa ajili ya kumkaribisha mpenzi wako.


1: Tandika shuka la rangi nyekundu katika kitanda chako, hakikisha shuka liwe na umbo la moyo ili kuwasilisha vizuri ujumbe wa upendo kwa mtu unayempenda.

2: Weka maua mekundu ya waridi kila sehemu inayoonekana kuanzia kitandani, sakafuni na hata kwenye sofa kwa lengo la kumpa ushawishi wa maongezi kuwa mazuri.

3: Washa mishumaa ya rangi nyekundu katika maeneo maalumu kama juu ya meza na pembe za ukuta kama ishara ya kumkaribisha kwa mahaba mazito na yenye msisimko.

4: Kama una redio, basi ni wakati wako kupiga muziki laini kwa sauti ya chini kwa ajili ya kukifanya chumba kuwa katika utulivu zaidi na tafakari pana.

# KATUNI



KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
MUME WANGU ACHA UBISHI, NJIA UNAYOTAKA KUPITA USIENDE KUNA WAKABAJI!
MH! INAWEZA KUWA AFADHALI YA HUKO!
SHEMEJI YAKO NIMEMPA TALAKA KAONDOKA IVI PUNDE NIMEMRUHUSU AOLEWE NA YEYOTE!
'THIBITISHA' 'HUTORUSHA NGUMI?
DEREVA POLEPOLE KUNA WATOTO HUMU!
WAMESHUKA HAJAWAONA TEMBEA BABA!
DEREVA UNA-TAKA TUACHE KUPAMBANA NA KORONA TUPA-MBANE NA WEWE?
USIZANI SIFA UTA-TUUA!
NNA HOMA
SURA LAKE BAYA LINAONYESHA NI MRAIBU WA DAWA ZA KULEVYA!
TUFE TU... WENGINE TUNA MADENI HADI BASI
FRESH TU!
MTA-ISOMA
HII DAWA YA UTAJIRI UTAJENGA GOROFA
KAMA HILI?
KAKA NAKUONA UNAPIGA MLUZI
HAPANA NAPIGA MBIZI
PISI KALI KAMA MIE WAKULETEWA MKE MWENZA? UCHURO
MZEE BABA MAISHA BILA 'HESABU' HAYAENDI
HILO SOMO NILIFELI
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...TIKITAKA NA MSULI UKWENI!

HABARI KIMATAIFA

# Rais Macron akataa kupimwa Covid-19 alipozuru Urusi

**MOSCOW,** URUSI

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron, amekataa kufanyiwa vipimo vya Covid 19 nchini Urusi kabla ya mkutano wake na mwenyeji wake Rais Vladimir Putin.

Taarifa iliyothibitishwa na Ikulu, ilieleza uchunguzi huo ulihitaji itifaki ya afya ambayo haikubaliki na haiendani na ratiba ya kiongozi huyo wa Ufaransa.

Hatua hiyo inafuatia ripoti kwamba Macron alikataa kipimo cha PCR kwa hofu kwamba Warusi wangepata DNA yake.

Viongozi hao baadaye walifanya mkutano huku wakiwa wamekaa mbali siku ya Jumatatu.

Viongozi hao hawakusalimiana kwa mikono na kukaa meza yenye urefu wa mita nne kati yao, huku waangalizi wakishangaa kama Putin alikuwa akiitumia njia hiyo kutuma ujumbe wa kidiplomasia.

Hata hivyo, vyanzo vya kidiplomasia vya Ufaransa viliiambia Reuters, kwamba Macron alikuwa ameambiwa achague kati ya kukubali vipimo vya PCR vya Urusi ili kuwa karibu na Putin au kutii sheria kali za kukaa mbalimbali.

"Tulijua vizuri kwamba hatua hiyo ilimaanisha kwamba hakutakuwa na kusalimiana kwa mkono katika meza hiyo ndefu. Lakini hatukubali waweze kupata DNA ya rais," moja ya vyanzo hivyo aliambia Reuters.

Chanzo hicho hakikueleza jinsi huduma hiyo ya ujasusi wa Urusi ingetumia DNA ya Macron katika masuala mengine.

Ikulu ya Kremlin ilihibitisha kwamba kiongozi huyo wa Ufaransa alikaa mbali na Rais wa Urusi kwa sababu alikataa kufanyiwa vipimo.

Msemaji wa Kremlin Dmitry Peskov, alisema Urusi inaelewa uamuzi huo wa Ufaransa na haikuathiri mazungumzo.

Macron alifanya vipimo vya PCR kabla ya kuondoka Ufaransa na daktari wake alifanya vipimo walipofika Moscow , chanzo kingine cha kidiplomasia kiliambia Reuters.

Kwa miongo kadhaa, majasusi wamewaorodhesha viongozi wa kigeni wakijaribu kuelewa utu wao, jinsi wanavyoweza kuitikia hali fulani na muda gani wanaweza kudumu madarakani. Sehemu ya hayo ni kuelewa afya zao.

Lakini maendeleo katika sayansi yanamaanisha kuwa sampuli moja ya DNA sasa inaweza kufungua kubaini siku za nyuma, sasa na hata za siku zijazo za mtu husika na kama anaficha ugonjwa au hali fulani au anaweza kukabiliwaje.

Macron sio kiongozi pekee aliyepewa diplomasia ya kukaa katika meza ndefu ndani ya Ikulu hiyo, mapema mwaka huu, Waziri Mkuu wa Hungary, Viktor Orban na Rais wa Irani Ebrahim Raisi pia walionekana wameketi mbali na Putin wakati wa ziara yao nchini humo.

Ikulu ya Kremlin imechukua hatua za tahadhari zaidi kumlinda kiongozi huyo ambaye baadaye mwaka huu anafikisha miaka 70 na ambaye amepewa chanjo ya Urusi ya Sputnik V, ili asiambukizwe.

Hata hivyo, siku tatu tu baada ya kukutana na Macron, Rais Putin alimkaribisha kiongozi wa Kazakhstan Kassym-Jomart Tokayev. Hata hivyo wawili hao walipeana mikono na kukaa kando ya meza ndogo ya kahawa kati yao.

Wakati wa mkutano wao Macron na Putin walizungumza kwa saa tano kuhusu mvutano kuhusu Ukraine.

Nchi za Magharibi zinasema Urusi inaweza kuivamia Ukraine lakini taifa hilo linakanusha kupanga na kufanya hivyo licha ya kuwa limekusanya wanajeshi zaidi ya 100,000 kwenye mpaka wake na Ukraine.

**BBC**



Marais Emmanuel Macron wa Ufaransa na mwenyeji wake Vladmir Putin wakiwa wamekaa kwa hatua kubwa baada ya kiongozi huyo kukataa vipimo vya Covid 19 vya Urusi. **PICHA: RFI**

# Biden, Putin kujadili kuepusha vita Ukraine

**WASHINGTON,**

MAREKANI

RAIS wa Marekani, Joe Biden na mwenzake wa Urusi Vladimir Putin, walitarajiwa kufanya mazungumzo kwa njia ya simu jana kujadili mzozo baina ya Ukraine na Urusi.

Wakati mazungumzo hayo yanafanyika, mataifa ya Magharibi yameonya kuwa vita huenda vikatokea wakati wowote. Kwa mujibu wa Ofisa mmoja wa Ikulu ya Marekani, Putin alitaka mazungumzo hayo yafanyike siku ya Jumatatu lakini Biden, akaomba yafanyike mapema kufuatia wasiwasi wa Marekani kuhusu uwezekano wa Ukraine kushambuliwa.

Australia na New Zealand zimeungana na mataifa mengine kuwataka raia wao kuondoka Ukraine kufuatia kitisho hicho. Hata hivyo, Urusi imekanusha madai ya Marekani kwamba inalenga kuishambulia Ukarine na ilisema wanajeshi wake takriban 1000 walioko karibu na mpaka wa Ukraine ni kwa ajili ya kulinda usalama wa Urusi dhidi ya uchokozi wa wanajeshi wa Jumuiya ya kujihami NATO.

**DW**

# Libya yaingia kwenye mzozo wa madaraka

**TRIPOLI,** LIBYA

MZOZO wa kugombea madaraka umeibuka nchini Libya, baada ya wabunge kumchagua Waziri Mkuu mwingine, Fathi Bashagha, siku ya Alhamisi.

Kutokana na uchaguzi huo, nchi hiyo sasa ina Mawaziri Wakuu wawili, baada ya Abdul Hamid Dbeibah, anayeongoza serikali ya umoja, kuapa kutokabidhi madaraka kwa kiongozi huyo mpya.

Hata hivyo, jumuiya ya kimataifa inamtaka Dbeibah kuendelea kuwa Waziri Mkuu hadi uchaguzi utakapofanyika.

Hayo yanajiri wakati Waziri Mkuu huyo wa serikali ya mpito akipinga hatua hiyo ya bunge akisema kuichagua serikali mpya ni jaribio jingine la kuingia Tripoli kwa nguvu.

Abdulhamid al-Dbeibah pia alitangaza nia yake ya kutogombea kwenye uchaguzi wa urais kwa lengo la kuufanikisha mpango huo, ingawa ameapa kubakia madarakani hadi hapo uchaguzi utakapofanyika.

Dbeibah aliyeahidi kuandaa mpango mpya wa kuutatua mzozo wa kisiasa nchini humo, alisema anaweza kuutangaza mpango wa serikali yake katika siku zijazo.

Wakati huo huo Waziri Mkuu mpya wa Libya, Fathi Bashagha, amewasili katika mji mkuu wa Libya, Tripoli. Bashagha aliyekuwa waziri wa zamani wa mambo ya ndani ya Libya, aliishukuru serikali ya GNU kwa juhudi zake na alisema anatarajia ushirikiano mzuri na kufanya kazi pamoja nayo.

**RFI**

# Ramaphosa asikitikia ongezeko la umasikini

**PRETORIA,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa, amesema kuongezeka kwa umaskini uliokithiri, ukosefu wa ajira, na kutokuwa na usawa ni hali isiyokubalika.

Ramaphosa alisema hayo wakati wa hotuba yake kuhusu hali ya kitaifa.

"Kama kuna kitu ambacho wote tutakubaliana, ni hali ya sasa ya nchi tuliyonayo ya umasikini mkubwa, ukosefu wa ajira na kutokuwa na usawa haikubaliki na haiwezi kuendelea," alieleza kiongozi huyo.

Kunahitajika nguvu za ziada ili kuwatoa mamilioni ya watu kutoka kwenye umasikini .

Afrika Kusini imejitahidi kubadilisha ukosefu wa usawa wa kiuchumi uliobuniwa chini ya utawala wa wazungu wachache.

Mwezi Julai mwaka jana ziliibuka hasira juu ya umasikini unaoendelea karibu miongo mitatu baada ya kumalizika kwa ubaguzi wa rangi.

Kufuatia ripoti za uporaji , uchomaji moto, zaidi ya watu 300 walikufa na kulitokea uharibifu wenye thamani kubwa ya pesa.

Ramaphosa pia alisema msaada wa kijamii ulioanzishwa mwanzoni mwa janga la dunia pia utaongezwa.

**VOA**

MAKALA

# HONGERA WIZARA YA ELIMU KATIKA HILI



Na Magabilo Masambu

**Pamoja na maoni hayo, wako pia ambao walionyesha wasiwasi kuhusu mpangilio wa mada za masomo. Hii ni kwa sababu mara nyingi walimu walikuwa wakichagua mada za kuanza nazo kutokana na urahisi au ugumu wa mada katika masomo yao.**

TANGU tumepata uhuru mpaka leo zaidi ya miaka 60, pamekuwapo na juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali pamoja na wadau wengine katika sekta ya elimu kuhakikisha taifa linakuwa na elimu bora na si bora elimu.

Lakini ni wazi kwamba changamoto za elimu bado ni kubwa kutokana na mabadiliko ya nyakati, ongezeko la watu na maendeleo ya sayansi na teknolojia mpya duniani, hivyo kwa namna yoyote ile, maboresho ya sekta ya elimu yataendelea kuwapo ili kuendana na kasi ya mabadiliko hayo.

Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere katika kitabu chake cha Elimu ya Kujitegemea (1967), anaeleza kwamba mwaka 1961 watoto wapatao 490,000 ndio walioandikishwa katika shule za msingi za Tanganyika ambao wengi walifika japo darasa la nne, wanafunzi 11,832 katika elimu ya sekondari na 176 pekee walikuwa kidato cha sita, yaani darasa la 14.

Mwaka huu wa 2022, kwa mujibu wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Innocent Bashungwa, tunao watoto 3,046,919 walioandikishwa shule za msingi pia mamia ya wanafunzi wa sekondari pamoja na vyuo vya kati na vyuo vikuu. Tafsiri yake ni kwamba tulipokuwa na watoto wachache, changamoto pia zilionekana kwa uchache, hivyo ni muhimu serikali kuendelea kushirikiana na wadau wa elimu katika kupokea maoni na ushauri namna ya kuboresha elimu yetu iwe katika soko la ushindani.

Katika maboresho hayo sasa, serikali imekuja na mpango wa kalenda ya masomo nchi nzima ambayo itatumika kama 'spidi gavana' ya ufundishaji katika shule za umma na binafsi zikijumuisha shule za msingi na sekondari.

Siku chache zilizopita, zimefanyika semina elekezi kwa walimu wa shule za msingi na sekondari kuhusu namna ya kutumia kalenda ya masomo itakayotumika nchi nzima katika kuhakikisha kwamba mada zote za masomo yote zitakuwa zikifundishwa kwa usawa kutokana na mwongozo wa kalenda hiyo.

Nilifanya mazungumzo na baadhi ya wawezeshaji wa semina na walimu waliohudhuria mafunzo hayo baadhi wakisema kalenda itawawezesha wanafunzi wenye uwezo wa chini na juu kupata uelewa wa pamoja kwa sababu hapatakuwa na suala la kukimbiza mada kitu ambacho kimekuwa kikiwapa nafuu wanafunzi wenye uelewa wa juu pekee. Lakini pia ikiwa mwanafunzi atahama shule A na kwenda shule B, alichokuwa akifundishwa alikotoka atakikuta alikohamia kuliko ilivyokuwa mwanzo ambapo ufundishaji ulipishana kutokana na mwalimu kuchagua mada za kuanza na kumalizia.

Pamoja na maoni hayo, wako pia ambao walionyesha wasiwasi kuhusu mpangilio wa mada za masomo. Hii ni kwa sababu mara nyingi walimu walikuwa wakichagua mada za kuanza nazo kutokana na urahisi au ugumu wa mada katika masomo yao. Lakini kwa sasa kutokana na matumizi ya kalenda, mwalimu atalazimika kufundisha mada kwa kufuata mpangilio uliowekwa badala ya kuchagua kutoka mada rahisi kwenda ngumu kama ilivyokuwa mwanzo.

Hezron Mwaipaja, Mwalimu katika Shule ya Sekondari Oldadai, Arusha, anasema: "Pamoja na mpango huu mzuri wa kalenda ya masomo, nafikiri kutakuwa na changamoto kidogo katika mpangilio wa mada maana mada hazilingani uzito. Ziko nyepesi na ngumu kwa hiyo katika ufundishaji ilikuwa vizuri zaidi kuanza na nyepesi ili kutowafanya wanafunzi kuona somo gumu.

"Pengine kwa sababu ndiyo tunaanza, tunaweza kutoa maoni huko mbele namna bora ya kuboresha zaidi. Pamoja na maoni ya wadau binafsi, niipongeze Wizara ya Elimu na wadau wote waliotoa mapendekezo haya ya kuwa na kalenda moja katika ufundishaji kwa sababu pamoja na kwamba itawafanya wanafunzi wasome kitu kimoja nchi nzima, kikubwa naiona kalenda hii kama jambo litakalowasaidia wanafunzi kuelewa zaidi masomo kuliko kukariri ili kufaulu mitihani pekee."

Upande wa pili utaratibu huu utawezesha mada zote kuisha kwa wakati na bila kutumia nguvu kubwa katika ufundishaji kwa sababu kila mada imepangiwa muda wake, japo inaonyesha pia kuna mada ambazo zinadhaniwa kuwa ndefu tofauti na muda uliowekwa ili kumalizika jambo ambalo litakuwa ndani ya uwezo wa mwalimu kuona namna gani anaweza kumaliza kwa wakati.

Mpango huu wa kalenda ya kitaifa katika ufundishaji ni mzuri kwa afya ya mwalimu pamoja na mwanafunzi mwenyewe. Tatizo ni kwa kiasi gani mpango huu utasimamiwa kuhakikisha unatumika kwa kila shule za binafsi na serikali. Isije kutokea kama michezo ya riadha uwanjani, mwanariadha mmoja kumshika shati mwenzake halafu akampita.

Nashauri kama tumeamua kutumia utaratibu mmoja nchi nzima, basi na iwe hivyo. Natambua kuwa elimu katika nchi na dunia kwa ujumla imekuwa biashara pengine wako watakaoona utaratibu huu utawachelewesha na kufanya kama ilivyokuwa mwanzo.

Hili ni jambo litakalohitaji ufuatiliaji wa karibu ili mwisho wa siku tupate wanafunzi watakaokuwa wanaelewa kuliko wanaofaulu mitihani kwa kukaririshwa na baada ya muda hawawezi kueleza na kujieleza.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Kikosi cha Zambia kilivyoangamia katika pwani ya Gabon



Na Adam Fungamwango

RUBANI Kanali Fenton Mhone aliyekuwa mchovu, aliyekuwa akiendesha ndege ya jeshi la Zambia, alizima mashine ya ndege hiyo baada ya injini moja kushika moto.

Hata hivyo, rubani alikosea. Badala ya kuzima injini ya upande ambayo ilikuwa ikishika moto, akazima injini nyingine iliyokuwa nzima, hali iliyofanya ndege aina ya DHC-5D Buffalo yenye namba za usajili AF-319 kupoteza mwelekeo na kuanguka, kabla ya kuzama kwenye bahari ya Atlantic karibu kabisa na pwani ya mji mkuu wa Gabon, Libreville.

Hiyo ilikuwa Aprili 27, 1993 ilipotokea ajali ya ndege ambayo ilikuwa na takriban watu 30, wakiwemo wachezaji wa timu ya taifa ya Zambia, benchi la ufundi na maofisa kadhaa.

Kikosi hicho kilikuwa njiani kwenda Senegal kwa ajili ya mchezo dhidi ya timu ya taifa hilo katika michezo ya hatua za mwisho ya kufuzu kucheza Kombe la Dunia mwaka 1994 nchini Marekani.

Kikosi hiki cha KK 11, kilikuwa na wachezaji wenye vipaji vya kipekee kwani mwaka 1988 wakati wa michuano ya Olimpiki, Seoul nchini Korea Kusini, iliwafunga Italia mabao 4-0.

Hakuna binadamu yeyote aliyepona kwenye ajali hiyo ila kuna baadhi ya wachezaji walinusurika na kifo hicho akiwamo Kalusha Bwalya aliyekuwa anachezea klabu ya PSV Eindhoven ya Uholanzi. Kalusha ambaye alikuwa nahodha, alipanga kutumia usafiri binafsi kutoka Uholanzi hadi Senegal kuungana na wenzake, huku Charles Musonda aliyekuwa anacheza klabu ya Anderlecht ya Ubelgiji hakwenda kutokana na majeraha.

Sasa ni miaka 28 imepita na ikifika Aprili 27 itakuwa miaka 29 lakini hakuna shabiki yeyote wa soka Afrika na dunia nzima aliyekuwa kijana au mtu mzima wakati huo asiyekumbuka tukio hili lililosikitisha na kuliza watu wengi.

Baada ya wananchi wa Zambia kuwa na huzuni na simanzi, nchi ya pili kwa mashabiki wake wa soka kuwa na huzuni kubwa ni Tanzania. Hiyo ni kwa sababu vifo vya wachezaji hao vilitokea miezi mitano tu baada ya kutoka nchini Tanzania kucheza michuano ya Kombe la Challenge na kuacha gumzo kubwa kutokana na kandanda lao safi waliloonyesha, wakiacha historia isiyofutika hadi leo.

Wachezaji walioangamia katika ajali hiyo ni Efford Chabala, John Soko , Whiteson Changwe, Robert Watiyakeni, Eston Mulenga, Derby Makinka, Moses Chikwalakwala, Wisdom Chansa, Kelvin Mutale, Timothy Mwitwa, Numba Mwila, Richard Mwanza, Samuel Chomba, Moses Masuwa, Kenan Simambe, Godfrey Kangwa, Winter Mumba na Patrick Banda.

Wachezaji hao wote walizikwa kwenye uwanja wa mpira ambao baadaye uliitwa Uwanja wa Taifa wa Mashujaa. Pamoja na kuchezewa mpira hadi sasa na kuingiza mashabiki 60,000, uwanja huo umekuwa kama sehemu ya utalii. Watu mbalimbali kutoka pande zote za dunia, hufika kuangalia makaburi ya mashujaa hao ambao mashabiki wengi wanaamini kama wasingepata ajali ile si tu kwamba Zambia ingefuzu kwenda Kombe la Dunia 1994 nchini Marekani, lakini pia ingetetemesha dunia kwa muda mrefu.

Mizimu ya wachezaji hao waliofia nchini Gabon iliwapa taifa lao Kombe la Afrika (AFCON) miaka 19 baadaye.

Michuano hiyo ilichezwa kwenye nchi hiyo hiyo ya Gabon na Zambia ikafanikiwa kutwaa ubingwa kwa kuifunga timu ya taifa ya Ivory Coast iliyokuwa na straika wa Chelsea aliyekuwa anatisha kipindi hicho, Didier Drogba. Iliishinda kwa mikwaju 8-7 ya penalti, baada ya kufuzu hatua ya nusu fainali, wachezaji na viongozi wa timu hiyo walitembelea eneo la pwani ambalo wenzao walianguka na ndege miaka 19 iliyopita. Dua na sala kwa marehemu na wao kujiombea hazikwenda bure.

"Tulitaka kushinda kombe hili ili wananchi wa Zambia wajivunie na kwa wale waliokufa, kupumzika kwa amani. Sasa roho zao zitakuwa na amani," alisema mchezaji wa timu hiyo, Felix Katongo, baada ya ushindi.

Jambo lingine ambalo lilikuwa la kihistoria katika michuano hiyo ambayo Zambia ilichukua ubingwa ni kwamba Kalusha Bwalya, ambaye alikuwa sehemu ya kikosi kilichoanguka na wachezaji waliokuwa kwenye ndege kufariki dunia, alikuwa Rais wa Chama cha Soka cha Zambia (FAZ).

Watanzania hawakisahau kikosi hicho kwa sababu kilifika nchini Novemba 1992, miezi mitano kabla ya kuangamia na kikapiga kambi jijini Mwanza kikiwa kwenye Kundi B na timu za Tanzania Bara, Malawi, Ethiopia na Zanzibar. Kundi A lilikuwa jijini Arusha na timu za Uganda, Tanzania Bara B, maarufu kama Kakakuona, Kenya na Shelisheli.

Ni michuano ambayo Uganda ilikuwa mabingwa kwa kuifunga Kakakuona bao 1-0, likifungwa na Issa Ssekatawa.

Pamoja na Zambia kutotwaa kombe, soka lake lilivutia wengi. Mechi ya kwanza iliichapa Ethiopia mabao 3-2, yakifungwa na Chikwakwala na Chomba akifunga mawili. Ilifungwa bao 1-0 dhidi ya Malawi, ambapo mechi za timu hizi mbili huwa hazitabiriki kwa sababu ni watani wa jadi kama Taifa Stars na Harambee Stars, huku mechi ya mwisho ya kundi ikifunga Tanzania Bara mabao 2-1 yote yakifungwa na Mutale. Zambia iliiadhibu Zanzibar mabao 8-0 yakifungwa na Mutale aliyepiga 'hat-trick', Banda akifunga mawili, Makinka mawili na moja Zanzibar wakijifunga wenyewe, kabla ya kutolewa hatua ya nusu fainali dhidi ya Uganda kwa mikwaju ya penalti 4-2.

# HADITHI

# Ajenda ya Siri-17

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

ILIKUWA vilio. Eddy sasa alianza kazi ya kuwabembeleza. Bi. Mtupeni ndiye aliyeanza. Binti yake Mwasi alifuatia. Baadaye Mzee Digalu, akaanza kufuta machozi. Ilikuwa kama alipeleka habari ya msiba.

Haikuwa hivyo. Alichowaambia ni kwamba, amemaliza kukusanya ushahidi kesi ya Tina, hivyo anatarajia kukata rufani ili isikilizwe tena kwenye Mahakama ya Rufani.

Vilikuwa vilio vya furaha na huzuni pia.

"Una uhakika atashinda kweli baba?"

"Hapana. Si kama atashinda ila tunataka haki itendeke. Tunataka wale walioshirikiana naye nao kama ushahidi utawatia hatiani, basi na wao waungane naye. Hicho ndicho kilichonivuta mimi kuiingilia kesi hii. Na kilichonisukuma mimi ni kilio cha yule msichana Tina pale mahakamani siku ile. Kilio cha huyu wewe mama na binti yako. Iliniuma sana. Pia nilianza kuwa na shaka kama msichana kama yule anaweza kutekeleza mauaji yale bila msaada wowote wa watu wenye akili ya mambo yale," aliwaambia.

Wakati Bi. Mtupeni na binti yake wakiwa wamekumbatiana kwa vilio, wakionekana kumkumbuka Tina aliyehukumiwa kunyongwa. Mzee Digalu baada ya kufuta machozi kwa kitambaa alifunguka.


"Kijana sisi kama walezi wake, tunakutakia kila la kheri. Tunakupa baraka zetu zote kama ulivyokuja kuomba hapa. Ni kweli mpaka sasa hatujui ilikuwaje hadi amefanya hivyo. Nasi pia kama walezi wake tunataka kila kitu kiwe wazi. Hata kama atanyongwa, basi tujue nani na nani walihusika kumshawishi. Ni kweli yule mtoto mdogo hawezi kukurupuka kufanya hivyo. Tutakupa ushirikiano wote hadi mwisho na sisi tutakuja mahakamani kusikiliza kama ambavyo tulikuwa tunakuja mwanzo."

****************************

Jana yake ilikuwa siku ya furaha sana kwake. Ni siku ambayo alimpokea mpenzi wake nyumbani kwake Kijitonyama.

Si kama hakuwa anakuja mara kwa mara lakini siku hiyo Mwahija alilala kwa Eddy.

Awali ilikuwa anakuja tu na kuondoka. Hakuwa anaruhusiwa kulala nje na mama yake mdogo. Hakuwahi kufanya hivyo hata siku moja, tangu awasili Dar es Salaam, miaka miwili iliyopita akitokea Tanga.




**Hivyo ndivyo Eddy alivyopata fursa ya kupitisha usiku mzima nyumbani kwake akiwa na mpenzi wake aliyetokea kumpenda kwa muda mfupi tu, Mwahija.**

Mama yake mdogo alikuwa mkali pamoja na kwamba Mwahija alikuwa mfamasia na alikuwa anafanya kazi, analipwa mshahara na ana uwezo wa kupanga nyumba au chumba na kuendesha maisha yake mwenyewe.

Mama yake alikataa kukaa peke yake kwa sababu ni mtoto wa kike. Aliona kuruhusu mtoto wa kike kuondoka nyumbani na kuendesha maisha peke yake kama kumpa uhuru uliopitiliza kwa sababu huwezi kujua atautumia vipi uhuru huo. Kama mtoto wa kiume kweli, lakini wa kike ni tatizo.

"Unaweza kuletewa watoto wasio na baba hapa. Kuna wanaume wanapenda vya bure, anaweza kuja kwenye nyumba yako akasema anakupenda kumbe sababu anataka kukaa nyumba ya bure na kukutumia, halafu likija la kutokea anakukimbia." Hayo ni maneno alikuwa akiwaambia mabinti zake mwenyewe nyumbani kwake Tegeta pamoja na binti wa dada yake, yaani Mwahija.

"Hapa kutoka nyumbani na kwenda kuishi kwingine ni mpaka uolewe. Siwezi kuwakataza kuwa na uhusiano kwa sababu nyinyi ni wakubwa, lakini mpaka huyo mtu nimwone mimi mama yenu mkubwa sasa. Nikimwona tu mtu mara moja, mbili tatu, najua huyu ana nia nzuri si mbabaishaji.

Naweza hata kuruhusu siku ukaenda naye usiku mmoja lakini lazima awe amekuja hapa kuweka dhamana. Chochote kitakachotokea, basi awajibike."

Na hivyo ndivyo ilivyotokea kwa Eddy. Baada ya mapenzi yao kuwa motomoto, Mwahija alimpeleka kwa mama yake mdogo. Mwonekano, heshima na ucheshi wake, ulimfanya mama yake mdogo Mwahija, Bi. Mwanabakari kumwamini Eddy kuliko hata mwenye mpenzi wake.

"Mwanangu pale umepata. Ukisikia mwanamume ndiyo huyu. Kwanza ana heshima, mpole, mcheshi, sijui vingine, utajua wewe mpenzi wake, labda anapiga, au ana wivu sana. Lakini kwa mimi ninavyomwona, hapa mama, ushindwe mwenywe."

"Mhh, mama, ya kweli hayo?" Mwahija alimuuliza mama yake mdogo kiuzushi.

"Mimi pia nilikuwa msichana kama ninyi, namjua mwanamume bora na mbabaishaji hata kwa kumuangalia tu."

"Ni kweli mama, miezi mitatu tangu niwe naye, kusema kweli imekuwa ya furaha sana. Sijawahi kuwa na furaha kwenye maisha yangu kama nilivyokutana na huyu baba. Kwangu ni mpenzi rafiki. Pamoja na kuwa mpenzi wangu, tukiwa pamoja utafikiri mtu na rafiki yake. Tutacheza, tutataniana, atanichekesha hapo, yaani hakuna siku ukikaa naye utaboreka."

"Eeeeeh, mtoto weee." Mama alichombeza wote wakaangua kicheko.

Hata siku Eddy alipokuja kumwomba Mwahija kikubwa kwa mama yake mdogo, hakukuwa na pingamizi kubwa.

Alichomwambia mama ni kwamba anamchukua kwenda naye kwenye sherehe ya ndugu yake na angemrudisha kesho.

"Arudi kweli kesho huyo mkwe, si zaidi ya hapo." Akatoa angalizo naye akajibu: "Ndiyo mama, ahsante sana."

Hivyo ndivyo Eddy alivyopata fursa ya kupitisha usiku mzima nyumbani kwake akiwa na mpenzi wake aliyetokea kumpenda kwa muda mfupi tu, Mwahija. Msichana mfamasia anayefanya kazi kwenye duka la dawa la 'Ni Sisi Pharmacy' lililopo Tegeta, Dar es Salaam.

Alimpata kwa bahati tu. Ni wakati anafuatilia kesi aliyojipa kazi ya kuipeleleza. Ni kesi ya mauaji iliyomkabili binti wa miaka 18, Tina Kauzeni, msichana hausigeli dhidi ya bosi wake Hafidh Chilambo na kuhukumiwa kunyongwa mpaka kufa.

Upelelezi wake wa kutaka kujua kama binti huyo alifanya mauaji hayo mwenyewe, alilazimishwa au alisaidiwa na watu ambao wako nyuma ya pazia, lakini wameshindwa kupatikana. Baadhi wanadai kuwa huenda wafanyabiashara wenzake Chilambo wako nyuma ya hili.

Kati ya watu wote waliotoa ushahidi, Eddy hakuona mwingine wa kuanza naye, isipokuwa mfamasia ambaye alikwenda kutoa ushahidi aliyemuuzia dawa ambazo zilikatisha uhai wa mfayabiashara huyo. Kazi ikazaa mapenzi. Eddy akayatumia pia mapenzi hayo kwenye kazi.

Ndiyo maana hadi wakati huo Mwahija akawa anamfahamu Eddy kwa jina la Danny na anachojua ni mjomba wa Tina. Hata alipoombwa msaada wa kutafuta mahali ambapo mlinzi wa zamani wa nyumba hiyo wakati mauaji yanafanyika, Mwahija alifanya hivyo akijua anayemtafutia ni mjomba wa Tina.

Alilipata jina la Mzee Kalango na mahali anapoishi Goba. Akamkabidhi Dan kwa anavyomjua yeye, ambaye pia kwa sasa ni mpenzi wake. Bila kujua huyo ni mpelelezi mashuhuri nchini na Afrika kwa ujumla, Eddy Kamal.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# HAKUNA MWENYE MANENO NA BSS

HATIMAYE mshindi wa shindano la Bongo Star Search (BSS) Bryson Yohana, amekabidhiwa zawadi yake ya Shilingi milioni 20, jana hivyo kuondoa mashaka kama ilivyokuwa kipindi cha nyuma.

Madam Rita alimkabidhi kiasi cha Sh. milioni 10, ambayo imetolewa na kampuni ya Startimes ili kukamilisha kiasi hicho baada ya Benki ya CRDB kutoa kiwango kama hicho juzi.

Awali shindano hilo lilikuwa likilalamikiwa kutotoa zawadi kwa washindi kiasi ambacho ilibidi serikali kuingilia kati.



# ROTIMI

## ATAMBULISHA 'WEAPON' KIBABE

WAKATI Vanessa Mdee amekuwa nyuma ya kinasa sauti kwa muda mrefu, mume wake Rotimi, ameachia video ya kibao chake kipya kinachoitwa Weapon.

Rotimi katika wimbo huo amemshirikisha msanii wa Nigeria Fireboy, ambao umeonekana kufanya vizuri tangu ulipotambulishwa siku nne zilizopita.

Rotimi na Vanessa ambao maisha yao wameyahamishia Marekani wamebahatika kupata mtoto katika uhusiano wao.

# Nuh Mziwanda bado ana mengi ya Shilole

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Nuh Mziwanda, amesema hataki kugombana na Roomy ambaye ni mume wa Shilole kwa sababu anachozungumza kuhusu mpenzi wake huyo wa zamani yana ukakasi.

Akizungumza katika kipindi cha Empire cha EFM radio, Mziwanda amesema kumtaja Shilole si kwamba anatafuta kiki, bali ni sehemu yake ya kuzungumza kuondoa dhana mbaya kwa watu kuwa wao ni maadui.

"Namuomba radhi Rommy kama atakuwa anakerwa na kile ninachoongea kuhusu mkewe, lakini atambue kuwa ninachosema sio kwa ubaya kutaka wao wagombane au ndoa yao ivunjike, bali ni hisia zilizo baki moyoni mwangu," alisema Mziwanda.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**BARCA KUSAJILI MABEKI**
BARCELONA wanataka kusajili mabeki na pia wako tayari kumuuza mlinzi wa kulia wa Marekani, Sergino Dest mwenye umri wa miaka 21, ili kusaidia kumnunua mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 21.***(ESPN)***

**COULIBALY ANUKIA SPURS**
KLABU ya Tottenham Hotspur inapanga kuelekeza zaidi mkakati wake wa uhamisho kwa vijana wenye vipaji na wale walio kwenye mikataba inayoelekea ukingoni, huku kiungo wa kati Mfaransa Mamadou Coulibaly (18), ambaye yuko Monaco akifikiriwa. ***(Mail)***

**LEWANDOWSKI VS HAALAND**
MSHAMBULIAJI wa Bayern Munich na Poland, Robert Lewandowski anataka kuhamia Real Madrid, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 anaweza kuona hilo lingekuwa jambo la kipumbavu ikiwa timu hiyo ya Hispania itamsajili Erling Haaland wa Dortmund. ***(AS)***

**SANCHEZ MSHAHARA CHINI**
MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United na Arsenal, Alexis Sanchez mwenye umri wa miaka 33, anatazamiwa kuongezewa mkataba mpya na Inter Milan, lakini raia huyo wa Chile atalazimika kukatwa mshahara. (***Gazzetta dello Sport***)

**TURNER KUTUA ARSENAL**
ARSENAL wanatarajia kumsajili golikipa wa Marekani, Matt Turner mwenye umri wa miaka 27 kutoka New England Revolution kwa dau la pauni milioni 7.5. ***(Mail)***

**NDOMBELE: NINA DENI SPURS**
KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Tanguy Ndombele amesema kazi yake Tottenham Hotspur "haijaisha" baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka miaka 25 kurejea Lyon. ***(RMC Sport via Mirror)***

**SALIBA KUTUA WEST**
KLABU ya West Ham msimu wa joto inapanga kumsajili beki wa kati wa Arsenal na Ufaransa, William Saliba mwenye umri wa miaka 20, ambaye yuko Marseille kwa mkopo. ***(Jeunes Footeux via Sport Witness)***

**CARVALHO ATAJWA LIVERPOOL**
LIVERPOOL huenda ikafufua nia ya kumsaka, Fabio Carvalho msimu wa joto baada ya kukaribia kumsajili mshambuliaji huyo wa Fulham mwezi uliopita. ***(AS - in Spanish)***

**ZIDANE BADO AJIPANGA**
KOCHA wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane mwenye umri wa miaka 49 bado hajakubali kumrithi, Mauricio Pochettino kama kocha wa Paris St-Germain kwa sababu anasubiri kuona ikiwa Didier Deschamps ataachia jukumu lake kama kocha wa Ufaransa. ***(RMC Sport)***

**COSTA ALIIKATAA FLAMENGO**
WINGA wa Brazil, Douglas Costa mwenye umri wa miaka 31 amepuuzia mbali ombi la Flamengo na kukubali kujiunga na klabu ya MLS LA Galaxy kwa mkopo wa miezi sita kutoka Juventus. ***(Fabrizio Romano)***

**BOTMAN KUWEKWA SOKONI**
KLABU ya Newcastle itafufua nia yake ya kumsajili mlinzi wa Lille, Sven Botman mwenye umri wa miaka 22 ikiwa itaponea kushushwa daraja kutoka kwenye Ligi Kuu England msimu huu. ***(Athletic)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR AREJEA KUIPA NGUVU PSG

●●●Ni baada ya jeraha la maumivu ya kifundo cha mguu aliyopata...

**PARIS, Ufaransa**

NEYMAR anaweza kuwa sehemu ya kikosi cha Paris Saint-Germain kitakachocheza dhidi ya Real Madrid katika mchezo wa hatua ya 16 bora wa Ligi ya Mabingwa Ulaya utakaochezwa keshokutwa.

Nyota huyo wa Brazil amekuwa nje ya uwanja kutokana na jeraha la kifundo cha mguu tangu Novemba, mwaka jana.

Lakini alirejea mazoezini Alhamisi, siku tano tu kabla ya mtanange wa kwanza kati ya wababe hao wawili wa Ulaya pale Parc des Princes.

Neymar ambaye alitimiza umri wa miaka 30 wikendi iliyopita alitumia zaidi ya wiki sita na alikosa mechi 12 za timu hiyo yenye maskani yake katika mji mkuu wa Ufaransa, Paris.

Sergio Ramos anabakia kuwa na shaka na tatizo lake la mguu kuelekea mchezo huo dhidi ya klabu yake ya zamani.

"Ni mchezaji mkubwa ambaye anapenda kucheza dhidi ya timu kubwa," alisema Kocha, Mauricio Pochettino wakati wa mkutano na waandishi kabla ya mechi dhidi ya Rennes akimzungumzia Neymar.

"Lakini pia ni mchezaji ambaye amepitia hali ya majeraha, naamini ana nafasi kubwa ya kuwapo kwenye mchezo wa Ligi ya mabingwa Ulaya."

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI

BURNLEY
VERSUS
LIVERPOOL

1 | 9.23
X | 5.42
2 | 1.30

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ERIKSEN: NILIONDOKA DUNIANI DAKIKA TANO



**LONDON, England**

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen amefunguka kuhusu hofu yake kubwa ya kiafya katika michuano ya Euro 2020 na kurejea Ligi Kuu England akiwa Brentford.

Eriksen hajacheza soka la ushindani tangu alipopatwa na mshtuko wa moyo wakati wa mechi ya ufunguzi ya Euro 2020 ya Denmark dhidi ya Finland Juni mwaka jana.

Mchezaji huyo amesema hakuwapo katika ulimwengu huu kwa dakika tano kabla ya kutibiwa uwanjani na kisha kukimbizwa hospitalini na kufanyiwa uchunguzi wa kina uliopelekea kuwekewa kifaa cha kusaidia mapigo ya moyo (ICD).

"Niliondoka kwenye ulimwengu huu kwa dakika tano hadi walipopata mapigo ya moyo wangu," alisema Eriksen akiiambia BBC Sport.

"Ni jambo lisilo la kawaida katika ulimwengu, la kushangaza, kwa sababu ilitokea na nilikuwa mahali nilipokuwa, lakini kuona nilipo sasa ni jambo la kushangaza sana."

Alipoulizwa kama anakumbuka kilichotokea kabla ya kuanguka kwake dhidi ya Finland, kiungo huyo alijibu: "Ninaweza kukumbuka kila kitu isipokuwa dakika tano, kutupa ndani, mpira kugonga goti langu na kisha sijui nini kiliendelea.

"Baadaye niliamka na watu wakinizunguka na kuhisi shinikizo kwenye kifua changu, nikajaribu kurudisha pumzi yangu. Muda huo sikujua ni nini kilitokea halafu ikapita kichwani mwangu kuna kitu kilitokea katika miguu yangu.

"Niliweza kunyanyua mguu wangu juu, mambo madogo madogo niliyokuwa najaribu kuyafanya ili nione kilichotokea ndipo kwenye gari la wagonjwa nikasikia mtu akisema 'nilitoka kwa muda gani' na mtu akasema 'dakika tano' ndiyo ilikuwa mara yangu ya kwanza. Nilisikia kuwa nimeondoka."

Eriksen pia alitoa shukrani zake kwa wafanyakazi wa matibabu wa Denmark, wachezaji wenzake na maelfu ya mashabiki waliomwombea.

# Mtoto wa Ronaldo asajiliwa United




**MANCHESTER, England**

MTOTO wa Cristiano Ronaldo amemwaga wino kwenye mkataba mpya na Manchester United, akifuata nyayo za baba yake kwa kuwawakilisha miamba hao wa Ligi Kuu England.

Hatua hiyo imefikiwa mara baada ya kinda huyo mwenye umri wa miaka 11 kuonekana akifanya mazoezi na baba yake wakati wa mapumziko ya msimu wa baridi wa Ligi Kuu.

Ronaldo Jr alipigwa picha akiwa ameshika jezi yenye namba saba baada ya kukubali kuongeza muda wa kukaa na timu ya vijana ya United, kinda huyo alikuwa na mtoto mwingine anayejulikana kwa jina la Gabriel, kipaji kingine ambacho kinatabiriwa makubwa katika ulimwengu wa soka.

"Muda pekee ndio utakaoongea," alisema Ronaldo katika mfululizo mpya wa Netflix ya Georgina, mke wake, inayojulikana kama I Am Georgina. "Sitawahi kumshinikiza atafanya anachotaka.

Ronaldo aliwahi kusema mwaka 2020: "Tutaona kama mtoto wangu anaweza kuwa mchezaji mkubwa, ana kipaji ana kasi ya kukokota mpira vizuri lakini hiyo haitoshi."

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# WANAMICHEZO WAMLILIA ALLY SONSO, AZIKWA JIJINI

**Na Adam Fungamwago**

WANAMICHEZO mbalimbali nchini wameendelea kutoa masikitiko yao kufuatia kifo cha beki wa zamani wa Lipuli, Yanga, Kagera Sugar na Timu ya Taifa (Taifa Stars), Ally Mtoni 'Sonso', aliyefariki dunia juzi na kuzikwa jana mkoani Dar es Salaam.

Marehemu Sonso alizikwa jana kwenye makaburi ya Ndugumbi, Magomeni Makuti, Dar es Salaam.

Sonso ambaye hadi anafariki dunia alikuwa mchezaji wa Ruvu Shooting alifariki akiwa anauguza mguu kwa mujibu wa baba yake mzazi, Abdulkarim Mtoni.

Klabu ya Yanga kupitia mtandao wake wa kijamii wa instagram imesema imepokea kwa masikitiko taarifa za kifo cha mchezaji wao wa zamani.

"Tunasikitika kutangaza kifo cha sentahafu wetu wa zamani Ally Mtoni 'Sonso', kilichotokea kwenye Hospitali Taifa ya Muhimbili. Sonso atakumbukwa kwa mengi klabuni, ikiwamo ujasiri wake ndani ya uwanja, nidhamu pamoja na kujitolea kuipigania jezi ya timu yetu," ilisema taarifa ya Yanga.

Shirikisho la Soka Nchini (TFF), limesema kifo cha mchezaji huyo ni pigo kwa sababu mchango wake bado ulikuwa unahitajika.

"Mungu aiweke roho ya marehemu Ally Mtoni 'Sonso' mahali pema peponi, Amina."

Wachezaji wa timu mbalimbali za Ligi Kuu, nao wameandika maneno mbalimbali ya kuhuzunishwa na msiba wa nyota huyo ambaye alizaliwa mwaka 1990.

Baba mzazi wa mchezaji huyo alisema kifo cha kijana wake ni pigo kubwa kwa familia, lakini yote hayo ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu.

"Msiba ni faradhi na kuwapo duniani ni sunna, unapolipata unamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa sababu huo ni uamuzi wake, hakuna mwamuzi zaidi yake. Mwanangu alikuwa ni kijana mzuri, familia yangu ina pigo kubwa sana, alikuwa karibu na mama yake, mimi, watoto wake na wa kaka zake, basi Mwenyezi Mungu ameamua," alisema Mtoni.



Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia (mwenye kofia ya bluu), akiwa na wahariri wa michezo wa vyombo mbalimbali nchini walipotembelea Mradi wa Kituo cha Ufundi cha Kigamboni jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: TFF**

# TFF kuhamia Kigamboni, Tanga

**Na Isaac Kijoti, TANGA**

VITUO vya soka vinavyojengwa Kigamboni, Dar es Salaam na Mnyanjani jijini Tanga, vinatarajiwa kukamilika na kukabidhiwa ifikapo Februari 26, mwaka huu, baada ya ujenzi kuelekea hatua za mwisho, imeelezwa.

Katika vituo hivyo, ambavyo kila kimoja kinahusisha viwanja vinne vya soka, hosteli na mabweni, bwawa la kuogelea, gym na kiwanja cha mpira wa kikapu, katika awamu hii ya kwanza vitakabidhiwa viwanja viwili.

Akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari, ambao walitembelea miradi hiyo Dar es Salaam na Tanga juzi chini ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), mhandisi Yasinta Wilbert, alisema kwa sasa wapo katika hatua za mwisho kukamilisha viwanja.

Yasinta alisema kiwanja cha nyasi bandia kitakabidhiwa sambamba na majengo hayo, lakini kile cha nyasi asili, zitaanza kuoteshwa kuanzia Machi 5, mwaka huu na baada ya siku 45 zitakuwa tayari zimemea lakini kinaweza kuanza kutumika baada ya miezi mitatu hadi sita.

Kwa upande wa Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema katika awamu hii ya kwanza vitakabidhiwa viwanja viwili kimoja cha nyasi bandia na kingine cha nyasi asili, lakini mradi mzima unahusisha viwanja vinne vya soka. Karia alisema shirikisho hilo litaingia katika historia ya kuwa na vituo vya soka kama ilivyo Misri na Morocco ambayo vituo vyake vina viwanja tisa vya soka.

Naye Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidau, akizungumzia namna watakavyofanya kazi kuhakikisha vituo hivyo viwili vinaendeshwa kwa ufanisi mkubwa, alisema pindi vitakapokamilika mkurugenzi wa ufundi wa shirikisho hilo kituo chake cha kazi kitakuwa Tanga.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI


"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 13/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 1963 | Sivasspor vs Yeni Malatyaspor | 1.65 | 3.77 | 4.96 |
| 14:30 | 5101 | AC Milan vs Sampdoria | 1.41 | 4.80 | 7.00 |
| 16:00 | 2663 | Swansea vs Bristol City | 1.99 | 3.44 | 3.48 |
| 16:00 | 5396 | Alaves vs Valencia | 2.80 | 3.21 | 2.55 |
| 16:30 | 5798 | Panathinaikos vs Lamia | 1.38 | 4.15 | 9.08 |
| 16:30 | 5988 | Waalwick vs Feyenoord | 9.81 | 5.69 | 1.25 |
| 17:00 | 1147 | Slovacko vs Slavia Prague | 4.29 | 3.69 | 1.80 |
| 17:00 | 1446 | Burnley vs Liverpool | 9.23 | 5.42 | 1.30 |
| 17:00 | 1498 | Hajduk Split vs Slaven Belupo | 1.30 | 4.82 | 8.09 |
| 17:00 | 1645 | Clermont Foot vs St Etienne | 2.28 | 3.30 | 3.10 |
| 17:00 | 3205 | Verona vs Udinese | 1.85 | 3.61 | 4.11 |
| 17:00 | 3512 | Pogon Szczecin vs Zaglebie Lubin | 1.49 | 4.03 | 5.57 |
| 17:00 | 4443 | Angers vs Strasbourg | 3.04 | 3.34 | 2.29 |
| 17:00 | 4875 | Tottenham vs Wolverhampton | 1.66 | 3.69 | 5.39 |
| 17:00 | 5282 | Genoa vs Salernitana | 1.85 | 3.56 | 4.21 |
| 17:00 | 5306 | Sigma Olomouc vs Mlada Boleslav | 2.86 | 3.46 | 2.37 |
| 17:00 | 5509 | Empoli vs Cagliari | 1.98 | 3.76 | 3.46 |
| 17:00 | 5889 | Nantes vs Reims | 2.20 | 3.09 | 3.49 |
| 17:00 | 5932 | Newcastle vs Aston Villa | 2.70 | 3.35 | 2.55 |
| 17:30 | 5293 | Union Berlin vs Borussia Dortmund | 3.73 | 3.83 | 1.87 |
| 18:00 | 1400 | Union Saint Gilloise vs St Truiden | 1.43 | 4.45 | 6.53 |
| 18:00 | 4700 | UTA Arad vs Dinamo Bucuresti | 1.51 | 3.87 | 6.27 |
| 18:15 | 2940 | PAOK vs Atromitos | 1.30 | 4.93 | 9.66 |
| 18:15 | 5128 | Levante vs Betis | 3.36 | 3.61 | 2.06 |
| 18:30 | 1099 | FC Zurich vs FC Lugano | 1.79 | 3.64 | 4.13 |
| 18:30 | 2677 | Famalicao vs Moreirense | 2.08 | 3.36 | 3.36 |
| 18:30 | 5190 | FC Luzern vs FC Sion | 1.92 | 3.60 | 3.60 |
| 18:45 | 4099 | Ajax vs Twente | 1.11 | 7.87 | 18.69 |
| 19:00 | 1597 | Celtic vs Raith Rovers | 1.05 | 9.69 | 24.23 |
| 19:00 | 1620 | LASK Linz vs Austria Klagenfurt | 1.46 | 4.35 | 5.41 |
| 19:00 | 3823 | Kasimpasa vs Alanyaspor | 2.47 | 3.25 | 2.76 |
| 19:00 | 4065 | Trabzonspor vs Konyaspor | 2.00 | 3.36 | 3.61 |
| 19:00 | 5086 | Varzim vs Leixoes | 2.67 | 3.11 | 2.57 |
| 19:05 | 1274 | Lens vs Bordeaux | 1.48 | 4.58 | 5.78 |
| 19:30 | 2011 | Leicester vs West Ham | 2.76 | 3.51 | 2.43 |
| 19:30 | 2055 | NK Osijek-HNK Rijeka | 1.91 | 3.42 | 3.52 |
| 19:30 | 3332 | Hoffenheim vs Arminia Bielefeld | 1.51 | 4.39 | 5.78 |
| 19:30 | 3770 | Olimpija Ljubljana vs Maribor | 2.55 | 3.23 | 2.51 |
| 19:30 | 5058 | Legia Warszawa vs Warta Poznan | 1.54 | 3.86 | 5.20 |
| 20:00 | 3364 | Sassuolo vs Roma | 3.30 | 3.70 | 2.05 |
| 20:00 | 3513 | Birkirkara vs Sirens | 1.88 | 3.53 | 3.53 |
| 20:30 | 1339 | Olympiakos vs AEK Athens | 1.80 | 3.45 | 4.34 |
| 20:30 | 4636 | Brugge vs Charleroi | 1.66 | 4.05 | 4.44 |
| 20:30 | 5207 | Real Sociedad vs Granada | 1.42 | 4.49 | 7.59 |
| 22:45 | 3431 | Metz vs Marseille | 4.97 | 3.93 | 1.64 |
| 22:45 | 3856 | Atalanta vs Juventus | 2.79 | 3.23 | 2.55 |
| 23:00 | 1856 | Kfco Wilrijk vs Kortrijk | 2.76 | 3.40 | 2.39 |
| 23:00 | 4105 | Las Palmas UD vs Burgos | 1.71 | 3.34 | 5.11 |
| 23:00 | 4809 | Espanyol vs Barcelona | 4.23 | 3.70 | 1.81 |
| 23:30 | 5844 | FC Vizela vs Gil Vicente | 2.72 | 3.22 | 2.52 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumapili Februari 13, 2022
Nipashe



Neymar arejea kuipa nguvu PSG HABARI UK 21

# SIMBA YATAMBA ASEC HAWAPONI

Lengo ni kujiweka katika nafasi nzuri kwenye kundi lao lakini yakiri...

**Na Saada Akida**

WAWAKILISHI pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa, Simba wanatarajia kuikaribisha Asec Mimosas kutoka Ivory Coast katika mechi ya Kundi D ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Mgeni rasmi katika mchezo huo ni Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mussa Zungu,ambaye pia ni mwanachama wa klabu hiyo ya Wekundu wa Msimbazi.

Akizungumza jijini jana, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, alisema timu yake imejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo na wanatambua ni mechi ngumu kuicheza kwao kwa msimu huu.

Pablo alisema licha ya kuwakosa baadhi ya wachezaji wake nyota, ana matarajio waliokuwepo watafanya vizuri zaidi na kujiweka katika nafasi bora kwenye msimamo wa Kundi D.

"Tutawakosa baadhi ya wachezaji wetu, lakini hakutaathiri upande wetu kwa sababu tumejipanga vizuri kwenda kutafuta ushindi katika mchezo huu muhimu," alisema Pablo.

Nahodha wa Simba, John Bocco, alisema wako tayari na imara kuelekea mechi hiyo ya kimataifa na watakuwa makini kutafuta ushindi lakini pia kuzuia mashambulizi kutoka kwa wapinzani wao ili kuzibakisha pointi tatu nyumbani.

"Kocha Pablo amefanya majukumu yake, kazi kubwa imebaki kwetu kuhakikisha tunashinda mechi hii ili kujiweka katika mazingira mazuri katika kundi letu," alisema Bocco.

Selemani Matola, Kocha Msaidizi wa Simba na nahodha wa zamani wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, amesimulia namna timu hizo mbili zilivyokutana mara ya mwisho mwaka 2003 ikiwa ni baada ya kuwavua ubingwa Zamalek ya Misri.

"Mechi ilikuwa ngumu sana, nakumbuka hata maandalizi yake yalikuwa makubwa, tulikaa kwenye hoteli nzuri na kila kitu kilikwenda vizuri, nyumbani tulishinda bao 1-0, na tulihitaji ushindi ili tufuzu robo fainali lakini haikuwa hivyo, tulipoteza kwa mabao 4-3 ugenini, mechi ilikuwa ngumu, baada ya mchezo tulipongeza kwa kazi tuliyofanya kwa sababu Asec ilikuwa timu bora sana kipindi hicho," alisema Matola.



Mshambuliaji wa Simba, Pape Ousmane Sakho (kushoto), akiwania mpira dhidi ya mchezaji mwenzake wa timu hiyo katika mazoezi ya kujiandaa kuikaribisha Asec Mimosas katika mechi ya Kundi D ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika utakaochezwa leo jijini Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA SC**

Naye Kocha wa Asec Mimosas, Julien Chevalier, alisema wamejiandaa vizuri kwa ajili ya mchezo dhidi ya Simba na wamekuja kutafuta matokeo mazuri katika mchezo huo wa kwanza.

"Simba ni timu nzuri na ina uzoefu mkubwa katika michuano ya Ligi ya Mabingwa, mchezo utaleta ushindani mkubwa kwa sababu tumejiandaa kutafuta matokeo mazuri kama ilivyo kwa wapinzani wetu," alisema Chevalier.

Nahodha wa Asec Mimosas, Abdulkarim Cisse, alisema wanaifahamu Simba ni timu nzuri na wamekuja kupambana kutafuta matokeo mazuri katika mchezo huo.

## Rais Samia aendeleza neema kwa wasanii

**Na Shufaa Lyimo**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ametoa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya kuinua Mfuko wa Wasanii, awali alitoa kiasi kama hicho ili kuwasaidia wasanii wa hapa nchini.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, wakati alipokuwa anawaaga wasanii wa Tamthilia ya Huba inayorushwa na Kituo cha Televisheni cha DSTV muda mfupi kabla hawajaelekea Dubai walipoalikwa na wadau wa tamthilia hiyo.

Mchengerwa alisema uamuzi wa Rais Samia kuendelea kuchangia mfumo huo kila mwaka ni kutokana na kutambua thamani ya kazi wanazozifanya.

"Ninatambua mmefanya kazi kubwa kwa kutumia nguvu zenu binafsi, serikali inatambua mchango wenu, ninaomba mkautangaze zaidi utamaduni wetu," alisema Mchengerwa.

Aliongeza serikali itakuwa na wasanii bega kwa bega ili kuhakikisha wanafika mbali zaidi ikiwamo kuwapa mikopo isiyokuwa na riba pamoja na kufungua kituo cha redio na televisheni zitakazokuwa zinarusha kazi zao.

Aliwataka wasanii hao kwenda kuitangaza vizuri Tanzania kupitia kazi yao hiyo na kuwatakia kila la kheri katika safari yao.

Naye Rais wa Bodi ya Filamu Tanzania, Elia Mjata, alisema anaishukuru serikali kwa kuamua kushirikiana nao na anaamini watafikia malengo huku akitamba tamthilia hiyo imefanya vizuri kwenye ukanda wa Afrika Mashariki.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Huba, Aziz Mohamed, alisema tamthilia hiyo imefanya vizuri tangu mwaka 2016 hadi sasa na imesaidia kuwapatia ajira vijana mbalimbali.

"Kila kazi ina changamoto zake lakini pia tunashukuru kwa mafanikio tuliyoyapata ikiwamo hili la kualikwa na watazamaji nchini Dubai, tunakwenda kuutangaza vizuri utamaduni wetu," alisema Beny Kinyaiya kwa niaba ya wasanii wenzake walioigiza tamthilia hiyo.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, SL P 9